**KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU**

# MUONGOZO WA KUUFAHAMU UISLAMU KWA UFUPI NA KWA KUTUMIA VIELELEZO VYA PICHA

**I.A.Ibrahim**


## Wahakiki Kiujumla

Dr. William (Daoud) Peachy

Michael (Abdul-Hakim) Thomas

Tony (Abu-Khaliyl) Sylvester

Idris Palmer

Jamaal Zarabozo

Ali AlTimimi

## Wahakiki wa Kisayansi

Professor Harold Stewart kuofi

Professor F. A . State

Professor Mahjoub O. Taha

Professor Ahmad Allam

Professor Salman Sultan

Professor Msaidizi H. O. Sindi

**Kimefasiriwa na Mr. Zubeir Ndarawa,**
Mwanafunzi katika Kitivo cha Lugha na Ukalimani, Chuo Kikuu cha **Al-Azhar,**
Na ni Mwanachama wa Tanzania Students Union (TSU) Cairo. (A.R.E)

**Tafsiri imehakikiwa na:**

**Mr. Omari Juma Mangilile,**
Mwanafunzi katika Kitivo cha malezi na ualimu kiwango cha shahada ya pili (master) chuo kikuu cha Cairo,
Na ni Mwanachama wa Tanzania Students Union (TSU)
E_mail:mangilile@yahoo.com
Cairo. (A.R.E).

**Mr. Habshi Hassan,**
Mwanafunzi katika Kitivo cha Lugha na Ukalimani, Chuo Kikuu cha Al-Azhar,
Na ni Mwanachama wa Tanzania Students Union (TSU)
Cairo. (A.R.E)

Chini ya usimamizi wa Jumuia ya Tabligh Islamiya ya Misr
**P. O. BOX 834 Alexandrie Egypt**
**E_mail: info_en@islamic-message.net**
**cims_eg@yahoo.com**
**www.islamic-message.net**

**Kwa Ushauri au Maoni**

**Kama utakuwa na Ushauri au Maoni yoyote juu ya tafsiri ya kiswahili ya kitabu hiki au ungependa kujua zaidi kuhusu kitu chochote chenye kuhusiana na mambo ya kufasiri vitabu n.k tafadhali wasiliana na Mfasiri wa kitabu hiki Mr. Zubeir Ndarawa kwa anuani zifuatazo: ndarawa@hotmail.com au ndarawa@yahoo.com**
**Ahsanteni.**

**P. O. BOX 834 Alexandrie Egypt**
**E_mail: info_en@islamic-message.net**
**cims_eg@yahoo.com**
**www.islamic-message.net**

# YALIYOMO

**MAKALA** **UKURASA**


UTANGULIZI .............................. 6

SURA 1 .................................. 9

BAADHI YA VITHIBITISHO JUU YA UKWELI WA UISLAMU ......... 9

*(1) Miujiza ya Kisayansi ndani ya Qur'an Tukufu* ..................................9

A) Qur'an na ukuaji wa mimba: ..................................................10

B) Qur'an na Milima: ..................................................17

C) Qur'an na asili ya ulimwengu ..................................................20

D) Qur'an na Ubongo ..................................................23

E) Qur'an, Bahari na Mito: ..................................................25

F) Qur'an Bahari za vina virefu na Mawimbi ya ndani kwa ndani.................27

G) Qur'an na Mawingu ..................................................30

H) Maelezo ya Wanasayansi juu ya Miujiza ya kisayansi ndani ya Qur'an.....35

*(2) Changamoto Kuu ya Kuunda Sura Moja kama Sura za Qur'an Tukufu* .42

*(3) Utabiri wa Biblia juu ya kuja kwa Muhammad ﷺ, Mtume wa Uislamu* 44

1) Nabii kama Musa: ..................................................45

2) Ni miongoni mwa ndugu wa waizraeli: ..................................................46

3) Mwenyezi Mungu ataweka Maneno yake katika kinywa cha Nabii huyu:.......46

*(4) Aya za Qur'an Ambazo zimeeleza kutokea Matukio katika Siku za mbele na Kisha Yakatokea*..................................................47

*(5) Miujiza iliyofanywa na Mtume Muhammad ﷺ* ..................................49

*(6) Maisha ya hali ya chini ya Muhammad ﷺ*..................................49

*(7) Ukuaji wa ajabu wa Uislamu* ..................................54

BAADHI YA FAIDA ZA UISLAMU ........................................ 56

SURA 2 .................................. 56

*(1) Mlango wa Kuingia Peponi*..................................56

*(2) Wokovu wa Kuepukana na Moto*..................................58

*(3) Furaha ya Kweli na Amani Moyoni*..................................59

*(4) Msamaha wa Dhambi Zote Zilizotangulia*..................................60

SURA 3 .......................................... 62

MAELEZO YA JUMLA JUU YA UISLAMU .......................................... 62

*Uislamu Ni Nini?* .......................................... *62*
*Baadhi ya Misingi ya Imani ya Kiisilamu* .......................................... *62*
*Je kuna Chanzo Kitakatifu KingineZaidi ya Qur'an?* .......................................... *67*
*Mifano ya Maneno ya Mtume Muhammad ﷺ* .......................................... *68*
*Uislamu unasema nini kuhusu siku ya Kiyama?* .......................................... *69*
*Vipi Mtu atakuwa Muislamu?* .......................................... *72*
*Qur'an Inahusika na nini?* .......................................... *73*
*Mtume Muhammad ﷺ Ni nani?* .......................................... *74*
*Kusambaa kwa Uislamu Kumeleta Athari gani katika Maendeleo ya kisayansi?* .......................................... *76*
*Waislamu Wanaamini nini juu ya Yesu?* .......................................... *77*
*Uislamu Unasemaje kuhusu Ugaidi?* .......................................... *81*
*Haki za Binadam na Uadilifu katika Uislamu* .......................................... *83*
*Mwanamke ana Nafasi gani katika Dini ya Kiislamu?* .......................................... *86*
*Familia katika Uislamu* .......................................... *87*
*Waislamu Wanawatendea vipi Wazee?* .......................................... *87*
*Ni Zipi Nguzo Tano za Uislamu?* .......................................... *88*
*Uislamu Nchini Marekani* .......................................... *92*
*Kwa Maelezo Zaidi Kuhusu Uislamu* .......................................... *93*
*Kwa ushauri na maoni juu ya kitabu Hiki* .......................................... *95*
*Kwa kijisomea zaidi kuhusu Uislamu* .......................................... *96*
*Vitabu vya Marejeo* .......................................... *96*
*Nambari za hadithi* .......................................... *101*


✵ ✵ ✵

# UTANGULIZI

Kitabu hiki ni muongozo mfupi wa kuufahamu Uislamu. Nacho kina Sura tatu.

Sura ya kwanza, ‘‘**Baadhi ya vithibitisho juu ya ukweli wa Uislam,**’’ Sura hiyo inajibu baadhi ya maswali muhimu ambayo watu wanayauliza:

- Je ni kweli kwamba Qur’an ni maneno halisi ya Mungu, yaliyofunuliwa toka kwake ?
- Je ni kweli kuwa Muhammad ﷺ[1] ni Mtume alietumwa na Mungu?
- Je ni kweli kuwa Uislamu ni Dini ya Mungu ?



Katika sura hii, zimetajwa aina sita za ushahidi:

**1) Miujiza ya kisayansi ndani ya Qur’an tukufu: Sehemu** hii inazungumzia (kwa picha) baadhi ya hakika (facts) za uvumbuzi wa kisasa wa kisayansi zilizotajwa katika Qur’an tukufu, ambayo ilikwishafunuliwa karne kumi na nne zilizopita.

**2) Changamoto Kuu ya Kuunda Sura Moja kama Sura za Qur’an Tukufu:** Katika Qur’an, Mungu amewapa changamoto watu wote watunge sura moja iliyo kama sura za Qur’an. Tangu kufunuliwa kwa Qur’an, karne kumi na nne zilizopita, mpaka leo, hakuna mtu aliyeweza kuifikia changamoto hii,

1 Maneno haya ya kiarabu ﷺ. maana yake 'Mungu ampe rehema na amani'

ingawa sura ndogo sana ya Qur'an ni (sura ya 108) yenye jumla ya maneno kumi tu.

**3) Utabiri wa Biblia kuhusu kuja kwa Muhammad ﷺ, Mtume wa Uislamu:** Katika sehemu hii, kumejadiliwa baadhi ya utabiri wa Biblia kuhusu kuja kwa Mtume Muhammad ﷺ.

**4) Aya za Qur'an ambazo zimeeleza kutokea matukio katika siku za mbele na kisha yakatokea:** Qur'an ilielezea kutokea kwa Matukio siku za mbele na ambayo baadae yakatokea, kwa mfano ushindi wa Warumi dhidi ya Wafursi (Wairani).

**5) Miujiza iliyofanywa na Mtume Mohammad ﷺ:**

Miujiza mingi ilifanywa na Mtume Muhammad ﷺ Miujiza hiyo ilishuhudiwa na watu wengi.

**6) Maisha ya Hali ya Chini ya Muhammad ﷺ:** Hii inaonyesha wazi kuwa Muhammad ﷺ hakuwa mtume wa uongo aliedai utume ili apate kuchuma mali, ukubwa au madaraka.

Kutokana na aina hizi sita za ushahidi, tunahitimisha kuwa:

- Qur'an lazima itakuwa ni maneno hilisi ya Mungu, yaliyofunuliwa naye.
- Muhammad ﷺ ni Mtume wa kweli alietumwa na Mungu.
- Uislamu ni Dini ya kweli ya Mungu.

Ikiwa tunataka kufahamu kama dini ni ya kweli au ya uwongo, hututakiwi kutegemea miono yetu, mawazo, au tamaduni. Heri, tutegemee hoja na akili. Mungu alipowatuma mitume, aliwapa nguvu kwa miujiza na ushahidi ambao ulithibitisha kuwa wao ni mitume wa kweli waliotumwa na Mungu na kwa hiyo dini waliokuja nayo ni ya kweli.

Sura ya pili,‘‘**Baadhi ya Faida za Uislamu**,’’ inataja baadhi ya faida ambazo zinatolewa na Uislamu kwa kila mtu, kwa mfano:

1) **Mlango wa Kuingia Peponi**
2) **Wokovu wa Kuepukana na Moto**
3) **Furaha ya Kweli na Amani Moyoni**
4) **Msamaha wa Dhambi Zote Zilizotangulia.**

Sura ya tatu, **‘‘Maelezo ya Ujumla kuhusu Uislamu,**’’ inatoa maelezo ya ujumla kuhusu Uislamu, inasahihisha ufahamu potofu kuhusu Uislamu, na inajibu baadhi ya maswali yanayoulizwa mara mara, kama vile:

- Uislamu unasemaje kuhusu Ugaidi?
- Mwanamke ana nafasi gani katika Uislamu?

❊❊❊


## Sura 1

# BAADHI YA VITHIBITISHO JUU YA UKWELI WA UISLAMU

Mwenyezi Mungu amempa nguvu Mtume wake wa mwisho Muhammad ﷺ [1] kwa Miujiza mingi na Ushahidi mwingi ambao unathibithisha kuwa yeye ni mtume wa kweli alietumwa na Mungu. Vile vile Mwezi Mungu amekipa nguvu Kitabu chake alichokishusha mwisho, ambacho ni Qur'an tukufu, kwa Miujiza mingi ambayo inathibitisha kuwa Qur'an hii ni Maneno halisi ya Mungu, aliyoyafunua, na kwa hiyo Qur'an haijatungwa na mtu yeyote. Sura hii inajadili baaadhi ya ushahidi huo.

## (1) Miujiza ya Kisayansi ndani ya Qur'an Tukufu

Qur'an ni maneno halisi ya Mwenyezi Mungu, ambayo aliyashusha kwa Mtume wake Muhammad ﷺ, kwa kupitia Malaika Gabriel. Qur'an ambayo ilihifadhiwa na Muhammad ﷺ, naye akawasomea Qur'an hiyo wafuasi wake. Nao, kwa zamu, waliihifadhi, kuiandika, na kuipitia pamoja na Mtume Muhammad ﷺ. Zaidi ya hayo,



Qur'an Takatifu

[1] ﷺ ni neno la kiarabu lisomekalo rehema na amani zi mfikie.

Mtume Muhammad ﷺ aliipitia Qur'an pamoja na Malaika Gabriel kila mwaka mara moja na katika mwaka wa mwisho wa uhai wake Mtume ﷺ, waliipitia mara mbili. Tangu wakati iliposhushwa Qur'ani, mpaka leo hii, daima kumekuwepo na idadi kubwa nno ya Waislam ambao wamehifadhi Qur,an yote, neno kwa neno. Baadhi yao wameweza kuhifadhi nzima wakiwa na umri wa miaka kumi. Hakuna hata herufi moja ya Qur'an iliyobadilishwa ingawa karne nyingi zimepita.

Qur'an, iliyoshushwa karne kumi na nne zilizopita, imeelezea mambo ya hakika ambayo yamevumbuliwa au kuthibitishwa na wanasayansi hivi karibuni tu. Hii bila ya shaka inathibitisha kuwa Qur'an ni lazima itakuwa ni maneno halisi ya Mungu, yaliyofunuliwa naye kwenda kwa Mtume Muhammad ﷺ, na kwa hiyo Qur'an haikutungwa na Muhammad ﷺ au na mtu yeyote. Hii pia inathibitisha kuwa Muhammad ﷺ ni mtume wa kweli alietumwa na Mungu. Haingii akilini kuwa mtu yeyote wa miaka elfu moja na mia nne iliyopita angelijua hakika hizi zilizogunduliwa au kuthibitishwa hivi karibuni tu kwa kutumia nyenzo na njia za kisayansi za kisasa. Baadhi ya mifano inafuata.

## A) Qur'an na ukuaji wa mimba:

Katika Qur'an tukufu, Mwenyezi Mungu anaeleza kuhusu hatua za maendeleo ya ukuaji wa mimba ya binadamu:

**﴾Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo* Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti* Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe**

**mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji﴿[1]. Qur'an Sura ya 23 aya 12 hadi 14.**

Asili, ya neno *alaqah* ni la kiarabu lina maana tatu:
(1) Ruba (2) kitu kilichotundikwa na (3) Pande la damu ilioganda**.**

Kwa kulinganisha kati ya Ruba na Kiinitete (mimba changa), katika hatua ya *alaqah*، tunapata kuwa kuna kufanana kati ya vitu viwili hivyo,[2] kama tunavyoweza kuona katika umbo 1. Pia, kiinitete katika hatua hii kinapata virutubisho kutoka katika damu ya Mama, sawa sawa na ruba, ambaye anakula damu ya viumbe wengine.[3]

Maana ya pili ya neno *alaqah* ni Kitu kilichotundikwa. Na hivi ndivyo tunavyoweza kuona katika Umbo namba 2 na 3, utundikwaji wa kiinitete (mimba changa), katika hatua ya *alaqah* kwenye mfuko wa uzazi wa mama.

Na maana ya tatu ya neno *alaqah* ni pande la damu iliyoganda. Tunakuta kuwa umbo la upande wa nje wa kiinitete na mifuko yake, katika hatua ya *alaqah,* linafanana na pande la damu iliyoganda. Hii ni kwa mujibu wa kuwepo kiasi kikubwa cha damu iliyo katika kiinitete, katika hatua hii[4] (tazama umbo 4 ). Vilevile katika hatua hii, damu iliyo katika kiinitete haizunguki mpaka mwishoni mwa wiki ya tatu.[5] Kwa hiyo kiinitete katika hatua hii kinafanana na pande la damu iliyoganda.

---


[1] Tafadhali zingatia kuwa haya mabano maalumu ﴾ ﴿ katika kitabu hiki ni tafsiri tu ya maana ya ya Qur'an. na sio Qur'an yenyewe, kwani yenyewe imeandikwa kwa kiarabu. Toka Tarjuma ya Qur'ani Tukufu Kwa Kiswahili. Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani, unaweza kuipata katika Internet.
[2] Kitabu: *The Developing Human*, Moore and Persaud, 5th ed., p. 8.
[3] Human Development as Described in the Qur'an and Sunnah, Moore and others, p. 36.
[4] Human Development as Described in the Qur'an and Sunnah, Moore and others, p. 37-38.
[5] *The Developing Human*, Moore and Persaud, 5th ed., p. 65.

Kwa hiyo maana tatu za neno *alaqah* zinaafikiana na sifa za kiinitete kikiwa katika hatua ya *alaqah*.


Hatua inayofuata ambayo imetajwa katika aya hii ni hatua ya *Mudghah.* Neno la kiarabu *Mudghah* maana yake ni "kitu kilichotafunwa". Kama mtu akichukua bazoka[1] na kuitafuna mdomoni mwake kisha ilinganishwe na kiinitete kilicho katika hatua ya *Mudghah,* tutahitimisha kuwa kiinitete katika hatua ya *Mudghah* kiumbo, kinafanana na bazoka iliyotafunwa. Hii ni kwa kuwa umbo la uti wa mgongo wa mtoto akiwa katika hatua ya *Mudghah* linafanana kwa kiasi fulani na athari za meno katika bazoka iliyotafunwa.[2] ( tazama umbo 5 na 6)

Vipi Muhammad ﷺ angeweza kupata uwezo wa kufahamu mambo yote haya tangu karne kumi na nne zilizopita, wakati wanasayansi ni hivi karibuni tu ndio wamegundua yote hayo kwa kutumia vyombo vya hali ya juu na darubini zenye nguvu ambazo hazikuwepo wakati ule? Hamm na Leeuwenhoek walikuwa ni wanasayansi wa mwanzo kugundua viini vya mbegu za uzazi za Mwanadamu (*Spermatozoa*) kwa kutumia darubini zenye kiwango cha hali ya juu mwaka 1677 (zaidi ya miaka 1000 baada ya kufariki Muhammad (S.A.W.). Nao kwa bahati mbaya walidhani kuwa kiini cha mbegu za uzazi za binadamu kina kijimtu kidogo dogo ambacho hukua wakati kinapowekwa katika eneo la mfumo wa uzazi wa mwanamke[3].


[1] Bazoka, Ubani wa kutafuna, bigijii, Gum
[2] *The Developing Human*, Moore and Persaud, 5th ed., p. 8.
[3] *The Developing Human*, Moore and Persaud, toleo la tano, ukurasa wa 9.




***Umbo 1:*** *Michoro inaonyesha mfanano wa maumbo kati ya ruba na mimba ya binadamu katika hatua ya alaqah. (Mchoro wa ruba, umechukuliwa toka kwenye kitabu:''Human Development as Described in the Qur'an and Sunnah, Moore and others'' ukurasa 37, ambapo ulifanyiwa uboreshaji toka katika kitabu ''Integrated Principles of Zoology''Hickman and others. Mchoro wa Kiinitete, toka katika kitabu, Developing Huaman, Moore and Persaud, toleo la tano ukurasa wa 73.)*





***Umbo 2:*** *Tunaona katika mchoro huu, uning`iniaji wa kiinitete katika hatua ya alaqah ndani ya fuko la uzazi la mama.*
*(The Developiung Human, Moore and Persaud) Toleo la Tano Ukurasa wa 66.)*





***Umbo 3:*** *Katika picha hii ndogo, tunaona uning`iniaji wa mimba (wenye alama B) katika hatua ya alaqah (kiasi cha umri wa siku 15) katika fuko la uzazi wa mama. ukubwa halisi wa mimba ni 0.6 mm. (TheDeveloping Human, Moore, Toleo la 3 ukurasa wa 66, kutoka katika kitabu, Histology, Leeson and Leeson.)*

**Umbo 4**: *Mchoro asilia wa mfumo wa moyo na mishipa ya mimba katika hutua ya alaqah. umbo la nje la mimba na fuko lake linafanana na pande la damu, kutokana na kiasi kikubwa cha damu iliyomo katika Kiinitete. (The Developing Human, Moore, toleo la tano, ukurasa wa, 65)*





**Umbo 5**: *Picha ya Kiinitete chenye umri wa siku 28 kikiwa katika hatua ya Mudghah. Mimba katika hatua hii kimaumbile inafanana na bazoka iliyotafunwa, kwa sababu umbo la mgongo wa mimba linafanana kwa kiasi fulani na alama za meno katika kitu kiliotafunwa. Ukubwa halisi wa mimba ni 4mm. (The Developing Human, Moore and Persaud, toleo la tano, ukurasa wa 82. toka kwa Professor Hideo Nishimura, Kyoto University, Kyoto Japan.)*



*Umbo 6: Tunapolinganisha umbo la mimba katika hatua ya mudghah, na kipande cha bazoka ambayo imeshatafunwa, tunapata kuwa kuna kufanana kati ya vitu viwili hivyo.*

***A)** Picha ya mimba katika hatua ya mudghah. Hapa tunaona umbo la mgongo wa Kiinitete linafanana na alama za meno (The Developing Human, Moore and Persaud, toleo la tano, ukurasa wa 79)*

***B)** Picha ya kipande cha bazoka iliyotafunwa.*




Professor wa Heshima mstaafu Keith L. Moore ni mmoja wa wataalamu wa sayansi mashuhuri sana duniani katika sekta za uchambuzi wa mwili (Anatomia) na, elimu ya uzazi[1], pia ni mtunzi wa kitabu kiitwacho *The Developing Human*, kilichotafsiriwa katika lugha nane. Kitabu hiki ni Marejeo ya kisayansi na kiliteuliwa na tume maalum nchini Marekani kama ni kitabu bora zaidi kilichotungwa na mtu mmoja. Dr. Keith Moore ni Professor wa Heshima wa Anatomia na Biolojia ya Cell, katika Chuo kikuu cha Toronto, Canada. Huko chuoni Toronto, alishika nafasi ya msaidizi wa mkuu wa kitengo cha Utabibu sehemu ya *Basic sciences* na kwa muda wa miaka 8 alikuwa ni Mkuu wa kitengo cha uchambuzi wa

[1] Mimba, mbegu za uzazi, na mtoto kabla ya kuzaliwa.

mwili (Anatomia). Katika mwaka 1984, alipokea tunzo maalumu katika sekta ya anatomia nchini Canada, J.C.B zawadi kubwa inayotolewa na umoja wa wanatomia wa Kikanada) Ameshaongoza vyama mbalimbali vya kimataifa, kama vile Umoja wa wataalamu wa anatomia wa Kimarekani na Wakanada na Baraza la umoja wa wataalamu wa Elimu ya Biolojia.

Mnano mwaka 1981 katika mkutano wa saba wa tiba mjini Dammam, Saudi Arabia, Professor Moore alisema: Imekuwa ni furaha kubwa kwangu kusaidia kubainisha juu ya maelezo ya Qur'an kuhusu ukuaji wa binadamu. Ni wazi kwangu ya kuwa maelezo haya ya Qur'an ni lazima yatakuwa yamemjia Muhammad kutoka kwa Mungu, kwasababu karibu ya Elimu yote hii ilikuwa haijavumbuliwa hadi baada ya karne nyingi. Hii inanithibitisha kuwa Muhammad lazima atakuwa ni Mtume wa Mungu.[1]

Kufuatana na hayo, Professor Moore aliulizwa swali lifuatalo: ''Je maelezo hayo yanamaanisha kuwa wewe unaamini kuwa Qur'an ni Maneno ya Mungu?'' Alijibu: ''sioni uzito kukubali hivyo."[2]

Katika moja ya mikutano, Professor Moore alieleza, "....kwa sababu hatua za kiinitete cha mwanadamu zinachanganya (zina hali nyingi na ngumu kuzifahamu) kutokana na matendo yanayoendelea ya mabadiliko katika kipindi cha ukuaji, inapendekezwa kuwa mfumo mpya wa uainishaji uendelezwe kwa kutumia maelezo yaliyotajwa ndani ya Qur'an na Sunnah (mambo aliyoyasema, fanya au aliyoyathibitisha Muhammad ﷺ. Mfumo uliopendekezwa ni mwepesi wenye kukusanya kila kitu na unaafikiana na Elimu ya uzazi ya siku hizi. Uchunguzi wa kina juu ya Qur'an na Hadith

---

[1] Asili ya maelezo haya ni *This is the Truth (videotape)*. Tembelea website: www.islamic-guide.com/truth Kwa kujipatiaa nakala ya mkanda huo au kujionea video clips za maelezo ya Professor Keith Moore moja kwa moja.
[2] This is the Truth (videotape).

(maelezo ya kutegemewa yalionukuliwa na wafuasi wa mtume Muhammad ﷺ yanahusu kile alichokisema, fanya au alichokithibitisha Muhammad ﷺ. Ndani ya miaka minne iliyopita umegundulika mfumo wa uainishaji viinitete vya wanadamu mfumo ambao ni wa kushangaza tangu uliporekodiwa katika karne ya saba A.D Ingawa Aristotle, muanzilishi wa elimu ya uzazi alitambua kuwa viinitete vya kuku hukua kwa hatua, aligundua hayo kutokana na uchunguzi wake juu ya mayai ya kuku mnamo karne ya nne B.C., hakutoa maelezo yoyote yaliyokamilika kuhusu hatua hizo. Kwa kadiri inavyofahamika kutoka kwenye historia ya elimu ya uzazi, ni machache yaliyofahamika kuhusu hatua na uainishaji wa viinitete vya wanadamu mpaka karne ya ishirini. Kwa mantiki hii, maelezo juu ya kiinitete cha mwanadamu katika Qur'an hayawezi kutegemea elimu ya kisayansi katika karne ya saba. Hitimisho la pekee la kiakili ni kuwa: maelezo haya yalifunuliwa kwa Muhammad ﷺ toka kwa Mwenyezi Mungu. Muhamad ﷺ asingeweza kujua maelezo hayo yaliyokamilika kwa sababu alikuwa ni mtu asiejua kuandika wala kusoma pamoja na kuwa hakupata kabisa mafunzo ya kisayansi."[1]

## B) Qur'an na Milima:

Kitabu kiitwacho Ardhi *(Earth)* ni kitabu cha kiada na ni marejeo ya msingi katikaa vyuo vikuu vingi duniani. Mmoja wa watunzi wawili wa kitabu hicho ni Professor wa Heshima Frank Press. Alikuwa mshauri wa mambo ya kisayansi wa rais wa zamani wa Marekani Jimmy Carter, na kwa muda wa miaka 12 alikuwa ni mkuu wa chuo cha sayansi cha taifa mjini Washington, DC (*National Academy of Sciences*). Kitabu chake kinaeleza kwamba milima ina


[1] This is the Truth (videotape). Tazama pambizo no. 1 uk. 11


mashina[1] yaliyochini. Mashina hayo yameingia kwa kina kirefu ndani ya ardhi, kwa hiyo, milima ina umbo kama kigingi (tazama umbo 7, 8, na 9).

Na hivi ndivyo Qur'an ilivyoeleza kuhusu milima. Mwenye Mungu amesema ndani ya Qur'an:

> **﴾Kwani hatukuifanya ardhi kama tandiko,? Na milima kama vigingi?﴿ Qur'an 78:6-7.**

*Umbo 7: Milima ina mashina ya kina kirefu chini ya uso wa ardhi. (Earth, Press and Siever, ukurasa wa 413.*





*Umbo 8: Sehemu ya kielelezo. Milima, kama vigingi, ina mashina ya kina yaliyoingia ardhini. (Anatomy of earth, Cailleux, ukurasa wa 220.)*

---

[1] *Earth*, Press and Siever, ukurasa wa 435. vilvile angalia *Earth Science*, Tarbuck and Lutgens, ukurasa wa 157




***Umbo 9:** Kielelezo kingine kinaonyesha namna milima ilivyo na umbo kama kigingi, kwa sababu ya mashina yake ya kina kirefu ( Earth science, Tarbuck and Lutgens, ukurasa wa 158.)*

Sayansi ya kisasa juu ya ardhi imethibitisha kuwa milima ina mashina yenye kina kirefu chini ya uso wa ardhi (*tazama umbo 9*) na kuwa mashina hayo yanaweza kufikia vimo virefu zaidi kuliko vimo vyake vya juu ya uso wa ardhi.[1] Kwa hiyo tamko linalofaa zaidi katika kuelezea milima kwa msingi wa maelezo haya ni neno 'kigingi'. Kwani sehemu kubwa ya kigingi kilichowekwa madhubuti inafichwa ndani ya uso wa ardhi.

Historia ya sayansi inatueleza kuwa nadharia ya milima kuwa na mashina ya kina kirefu ilitambulishwa mwaka 1865 na mwanaanga bora bwana George Airy[2].

Milima vilevile ina cheza duru kubwa katika kuimarisha uso wa ardhi. Inazuia tetemeko la ardhi.[3] Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴿Na kaweka katika ardhi milima ili ardhi isiyumbe yumbe nanyi. Na mito, na njia ili mpate kuongoka.﴾ Qur'an 16:15**

[1] The Geological Concept of Mountains in the Qur'an, El-Naggar, p. 5.
[2] *Earth*, Press and Siever, ukurasa wa 435. villevile tazama *The Geological Concept of Mountains in the Qur'an, ukurasa wa 5.*
[3] [3] *The Geological Concept of Mountains in the Qur'an, ukurasa wa 44- 45.*

Kadhalika, nadharia ya kisasa ya (plate tectonics) inaeleza kuwa milima inafanya kazi kama viimarisho vya ardhi. Elimu hii inayohusu kanuni za milima kama viimarisho vya ardhi imeanza kutambulika katika mfumo wa plate tectonics mwishoni mwa miaka[1] ya sitini 1960.

Je katika kipindi cha mtume Muhammad ﷺ kungekuwa na mtu yeyote anaejua maumbo ya hakika ya milima? Je kungekuwa na mtu yeyote anaeweza kudhani kwamba mlima mkubwa mno na imara ambao anauona mbele yake, kwa hakika umejitandaza kwenye kina cha ardhi na una mizizi kama wanavyohakikisha wanasayansi? Jiolojia ya kisasa imethibitisha ukweli wa aya za Qur'an.



## C) Qur'an na asili ya ulimwengu

Sayansi ya kisasa ya elimu ya muundo wa ulimwengu, uchunguzi na nadharia inaashiria kwa uwazi kuwa, katika kipindi kimojawapo cha wakati, ulimwengu wote ulikuwa si chochote ispokuwa ni wingu la 'moshi' (yaani uzito kama wa majimaji wa hali ya juu usiopitisha kitu na mtungo wa gesi za moto)[2]. Na huu ni msingi mmojawapo usio na ubishi wa elimu mpya juu ya ulimwengu. Kwa sasa wanasayansi wanaweza kuona nyota mpya zilizoundwa kutokana na mabaki ya moshi huo. (Tazama umbo namba 10 na 11). Nyota zinazotoa mwangaza tuzionazo wakati wa usiku zilikuwa kama ulivyokuwa ulimwengu wote, katika malighafi hiyo ya moshi. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

---

[1] *The Geological Concept of Mountains in the Qur'an, ukurasa wa 5.*
[2] The first Three Minutes, a Mordern View of the Origin of the Universe, Weinberg, pp. 94-105.

**❮Kisha akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi...❯ Qur'an, 41:11**

Kwa sababu duniani na juu mbinguni (jua, mwezi, nyota, sayari, kikundi cha nyota, nk.) vimeundwa kutokana na moshi uleule, Tunahitimisha kwamba dunia na mbingu zilikuwa kitu kimoja kilichoungana kikamilifu. Kisha kutokana na moshi huu wenye hali moja, viliumbwa na kutawanyika vikawa mbalimbali. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

**❮Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?❯ Qur'an, 21:30**



***Umbo 10:*** *Nyota mpya iliyoundwa kutokana na wingu la gesi na vumbi zito (nebula- yaani kundi la nyota au unyevunyevu1) ambayo ni mojawapo ya mabaki ya ule moshi uliokuwa ndio asili ya ulimwengu wote. (The Space Atlas, Heather and Henbest )*

[1] Jamii ya nyota nyingi ndogo kama wingu



***Umbo 11:*** *Wangwa wa nebula, ni wingu la gesi na vumbi, kipenyo chake ni kadiri ya miaka 60, ya kimwangaza[1] (umbali wa masafa ya vipimo vya sayari) wangwa huu unasisimuliwa na miale ya urujuani isiyoonekana ya nyota ambazo zimeundwa hivi karibuni zikiwa na ukubwa wake. (Horizons, Exploring the Universe, Seeds plate 9, from Association of Universities for Research in Astronomy, Inc.)*

Dr. Alfred Kroner ni mmoja wa wanajiolojia mashuhuri. Yeye ni Profesa wa jiolojia na ni mwenyekiti wa kitengo cha jiolojia katika taasisi ya Geoscience, chuo kiku cha Johannes Gutenberg, Mainz, Germany. Alisema: "Fikiria Muhammad amekuja kutokea wapi... nadhani kitu hicho, takribani haiwezekani kwamba angejua

[1] kwa kipimo cha kugawa kati toka mwanzo hadi mwisho wa wangwa ni kadiri ya umbali wa miaka 60 ya mwanganza (60 light years in diameter) vipimo vya masafa ya sayari toka moja hadi nyengine au umbali wa masafa ya sayari yenyewe

vitu kama asili ya hakika ya ulimwengu, kwasababu wanasayansi wamegundua hayo ndani ya miaka michache, kwa kutumia teknolojia ngumu na ya hali ya juu, na hiyo ndio kadhia[1]. Vilevile amesema: "Mtu asiejua chochote kuhusu fizikia ya nyukilia karne kumi na nne zilizopita nadhani, asingeweza kuwa katika nafasi ya kugundua hayo kutokana na akili yake mwenyewe, kwa mfano, dunia na mbingu zilikua na asili moja."[2]

## D) Qur'an na Ubongo

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an kuhusu mmoja wa makafiri mbaya sana ambae alimzuia Mtume Muhammad ﷺ kusali katika Kaaba (Msikiti wa Maka):

**﴾Kwani! Kama haachi, tutamkokota kwa shungi la nywele!. Shungi la uwongo, lenye makosa!﴿ Qur'an, 96:15-16**

Kwanini Qur'an imeeleza kuwa paji la uso ni ongo na ovu? Kwanini Qur'an haikusema kuwa mtu mwenyewe ndie muongo na muovu? Je kuna uhusiano gani kati ya paji la uso na uongo au uovu?


Kama tutaangalia fuvu la kichwa kwa upande wa mbele wa kichwa tutaona seheme ya ubongo wa mbele. (tazama umbo:12) Nini inatuambia Fiziolojia (elimu ya kujua kazi za vitu mbalimbali) [3] kuhusu kazi za sehemu hii? Kitabu kinachoitwa *Essentials of Anatomy & physiology ,(misingi ya elimu 'sayansi ' ya uainishaji na elimu ya kujua kazi mbalimbali)* kinaielezea sehemu hii kama ifuatavyo: "vichocheo na mitazamo ya haraka haraka ya kupangilia na kuanzisha matendo, hutokea katika sehemu ya mbele iliyo kama ndewe, sehemu ambayo ni eneo la mwanzoni. Hili ni eneo la

---

[1] Chanzo cha maelezo haya ni Mkanda wa kweli wa (video) tembelea www.islam-guide.com/truth ambapo unaweza kujipatia copy ya mkanda huu au kujipatia clips za maelezo ya Professor Alfred Kroner. Moja kwa moja.
[2] This is the Truth (video tape)
[3] Elimu ya kutambua tabia ya mtu usoni mwake

muungano wa tabaka la nje la ubongo..."[1] Vilevile hicho kitabu kinasema: (Miongoni mwa mambo yanayofungamana na ushiriki wa sehemu hiyo katika kuzusha vichocheo, pia inaaminika kuwa, eneo la paji ndilo kituo cha matendo ya uadui...."[2]

Kwa hiyo sehemu hii ya ubongo ndio muhusika wa mipango, vichocheo, na kuanzisha tabia nzuri au mbaya na ndio muhusika wa kusema uwongo au ukweli. Kwa hiyo, ni jambo madhubuti kuielezea sehemu ya mbele ya kichwa kuwa ni ongo na ovu wakati mtu anapoongopa au kutenda uovu, kama ilivyosema Qur'an na kuisifu sehemu hii kama ongo na kosaji pale mtu anapoongopa au kufanya makosa (...Shungi la uwongo, lenye makosa!) Qur'an, 96:16




*Umbo:12 maeneo ya utendaji kazi ambayo ni maeneo ya upande wa nusu duara ya kushoto ya tabaka la nje la ubongo. Sehemu ya mbele ya paji ipo mbele ya tabaka la nje la ubongo. (Essentials of Anatomy & physiology, Seeley and others, ukurasa wa 210)*


---

[1] Essential of Anatomy & Physiology, Seeley and others, p. 211. Pia tazama The Human Nervous System, Noback and others, pp. 410-411.
[2] Essential of Anatomy & Physiology, Seeley and others, p. 211.

Wanasayansi wamegundua matendo haya ya eneo la mbele la kichwa katika miaka sitini tu iliyopita, na hayo ni kwa mujibu wa profesa Keith L. Moore.[1]

## E) Qur'an, Bahari na Mito:

Elimu ya sayansi ya kisasa imegundua kuwa katika sehemu ambazo zinakutana bahari mbili tofauti kuna kizuizi kati ya bahari hizo. Hiki kizuizi kinazigawa bahari mbili hizo kwa namna ambayo kila bahari inakuwa ina hali yake ya joto, kiwango cha chumvi na mgandamizo.[2] Kwa mfano, maji ya bahari ya Mediterania ni ya uvuguvugu, chumvi nyingi na mazito kidogo, ukiyalinganisha na maji ya bahari ya Atlantiki. Wakati maji ya bahari ya Mediterania yanapoingia bahari ya Atlantiki kupitia mlima Gibraltar, huwa yanakwenda masafa ya mamia kadhaa ya kilomita ndani ya bahari ya Atlantiki katika kina cha takribani mita 1000 yakiwa na hali\tabia yake ya uvuguvugu, chumvi, na uzito mdogo. Maji ya bahari ya Mediterania yanaendelea kuthibiti kama yalivyo katika kina hiki[3] (tazama umbo13).




***Umbo 13:*** *Maji ya bahari ya Mediterania kama yanavyoingia bahari ya Atlantiki kupitia mlima Gibraltar, yakiwa na hali yake ya uvuguvugu, chumvi na uzito mdogo, kwa sababu ya kizuizi ambacho kinatenganisha kati ya bahari hizo. Joto lipo katika nyuzi joto za Celsius(C°) (Marine Geology, Kuenen, ukursa wa, 43 pamoja na ungezeko dogo).*

---

[1] Al-E' jaz al-Elmy fee al-Nasseyah (The Scientific Miracles in the Front of the Head), Moore and others, p. 41.
[2] Principles of Oceanography, Davis, pp. 92-93.
[3] Principles of Oceanography, Davis, pp. 93.

Ingawa kuna mawimbi makubwa, mikondo mikali na maji kupwa na kujaa katika bahari hizi, lakini hazichanganyiki au kukeuka, kizuizi hicho.

Qur'an tukufu imeeleza kuwa kuna kizuizi kati ya bahari mbili zenye kukutana, bahari hizo hazivuki kizuizi hicho. Mwenyezi Mungu amesema:

> **﴾Anaziendesha bahari mbili zikutane; Baina yao kipo kizuizi, zisiingiliane) (Qur'an, 55:19-20﴿**

Lakini wakati Qur'an inapozungumzia kuhusu kitenganishi kilcho kati ya maji baridi na maji chumvi, inaonyesha kuwepo kwa "kizuizi kigawacho" pamoja na kitenganishi. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴾Naye ndiye aliye zipeleka bahari mbili, hii tamu mno, na hii ya chumvi chungu. Na akaweka baina yao kinga na kizuizi kizuiacho﴿ Qur'an, 25:53**.


Mtu anaweza kuuliza, Kwanini Qur'an imetaja kuwepo kwa kinga ilipozungumzia kitenganishi kati ya maji baridi na maji chumvi, lakini haijakitaja ilipozungumzia kitenganishi kati ya bahari mbili?

Sayansi ya kisasa imegundua kuwa katika milango ya mito, ambapo maji baridi na maji chumvi yanakutana, hali, kwa kiasi fulani, huwa ni tofauti na ile inayopatikana katika sehemu za makutano ya bahari mbili. Imegundulika kuwa kinachotenganisha maji baridi na ya maji chumvi katika milango ya mito ni eneo la mteremko (pycnocline) lenye msongamano wenye alama maalumu usioungana inayotenganisha kati ya tabaka mbili hizo[1]. Sehemu hii

---

[1] Kitabu: *Oceanography*, Gross, ukurasa wa, 242. Vilevile angalia, *Introductory Oceanography*, Thurman, ukurasa wa, 300-301.

ya mtenganisho ina uchumvi chumvi tofauti iliyomo katika maji baridi na chumvi iliyomo katika maji chumvi.[1] (tazama umbo14)




***Umbo 14:** Kipande kilichokata kwa urefu, kinaonyesha uchumvichumvi (sehemu za elfu ‰ ) katika moja ya mlango wa mto. Hapa tunaona mtengano (sehemu ya kutengana) kati ya maji baridi na maji chumvi. (Introductory Oceanography, Thurman.Ukurasa wa 301. kukiwa na ongezeko kiduchu)*

Maelezo haya yamegunduliwa hivi karibuni tu, kwa kutumia vyombo vya kisasa vya kupimia joto, uchumvi chumvi, msongamano, kiwango cha uyeyukaji wa oxygen, n.k. Jicho la binadamu haliwezi kuona tofauti iliyopo kati ya bahari mbili zikutanazo, kiasi ambacho, hizo bahari mbili zinaonekana kwetu zikiwa kama bahari moja ya jinsi moja. Kadhalika, jicho la binadamu haliwezi kuona vigawanyo vya maji katika milango ya mito vigawanyo vilivyo vya aina tatu: maji baridi, maji chumvi na eneo la kutenganisha (sehemu ya kutengana).

## F) Qur'an Bahari za vina virefu na Mawimbi ya ndani kwa ndani

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:


**﴿Au ni kama giza katika bahari kuu, iliyo funikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu. Giza juu ya giza. Akiutoa mtu mkono wake anakaribia asiuone. Na ambaye Mwenyezi Mungu hakumjaalia kuwa na nuru hawi na nuru﴾ Qur'an,24:40.**

[1] : *Oceanography*, Gross, ukurasa wa, 244. na, *Introductory Oceanography*, Thurman, ukurasa wa, 300-301.

Aya hii imetaja giza lipatikanalo katika bahari za kina kirefu na bahari kuu, giza ambalo kama mtu atanyoosha mkono wake, hawezi kuuona. Giza katika bahari za kina kirefu na bahari kuu linapatikana umbali wa kina cha mita 200 na zaidi kuelekea chini. Katika kina hiki, takribani hakuna mwangaza (tazama umbo15). Chini ya kina cha mita 1000 hakuna mwangaza kabisa[1]. Binadamu haweza kupiga mbizi zaidi ya mita arobaini bila msaada wa manowari au vyombo maalumu. Binadamu hawezi kunusurika bila kusaidiwa akiwa katika sehemu za bahari kuu zenye kiza na kina kirefu, kwa mfano kina cha umbali ma mita 200.[2]

Wanasayansi wamegundua giza hili hivi karibuni kwa kutumia vyombo maalumu na manowari ambazo zimewawezesha kuzamia ndani ya vina vya bahari kuu.


*__Umbo 15__ :Kati ya asilimia 3 hadi 30 za mwangaza wa jua huakisiwa katika usawa wa bahari. Kisha takribani rangi zote saba za mtungo wa mwangaza hufyonzwa moja baada ya nyingine katika mita 200 za mwanzo, ispokua mwangaza wa buluu. (Oceans, Elder and Pernetta, ukurasa wa,27.)*




[1] Kitabu*:* ***Oceans****,* Elder and Pernetta, ukurasa wa 27.
[2] Submarines or special equipment.

Vilevile tunaweza kufahamu kutokana na sentesi zifuatazo katika aya iliyotangulia, (....katika bahari kuu, iliyo funikwa na mawimbi juu ya mawimbi, na juu yake yapo mawingu....) tunafahamu ya kwamba hayo ni maji ya kina kirefu cha bahari na bahari kuu yaliofunikwa na mawimbi, na juu ya mawimbi haya kuna mawimbi mengine, Na ni wazi kuwa seti ya pili ya mawimbi ndio mawimbi ya juu yaliyo katika usawa wa bahari tunayoyaona, kwa sababu aya inaeleza kuwa juu ya mawimbi ya pili kuna. mawingu. Lakini vipi kuhusu mawimbi ya kwanza? Wanasayansi hivi karibuni wamegundua kuwa kuna mawimbi ya ndani kwa ndani yanayotokea katika muingiliano wa mgandamizo uliopo kati ya tabaka zenye mvutano ulio tofauti tofauti[1]. (Tazama umbo 16) Mawimbi ya ndani kwa ndani yanafunika maji ya kina kirefu ya bahari ndogo na bahari kuu kwasababu maji ya kina kirefu yanamgandamizo wa juu zaidi kuliko mgandamizo wa maji yaliyopo juu yake. Mawimbi ya ndani kwa ndani yanatokea kama yanavyotokea mawimbi ya juu ya bahari. Pia mawimbi haya ya ndani kwa ndani yanaweza kupasuka, kama mawimbi ya juu ya bahari. Mawimbi ya ndani kwa ndani hayaonekani kwa macho ya binadamu, lakini yanaweza kugundulika kwa kuchunguza mabadiliko ya hali ya joto au chumvi chumvi ya sehemu husika.[2]

***Umbo 16****: Mawimbi ya ndani kwa ndani yakiwa katika muingiliano kati ya tabaka mbili za maji ya mgandamizo tofauti tofauti. Moja ni nzito (takaba ya chini), na nyingine ni nzito kidogo (tabaka ya juu). (Oceanography, Gross, ukurawa wa, 204)*




[1] *Oceanography*, Gross, ukurasa wa,205.
[2] Oceannography, Gross, p. 205.


## G) Qur'an na Mawingu

Wanasayansi wamechunguza aina za mawingu na wametambua kuwa mawingu ya mvua hujitengeneza na kujiunda kutokana na mfumo unaojulikana na hatau maalum ambazo hufungamana na aina maalum za upepo na mawingu.

Aina mojawapo ya mawingu ya mvua ni mawingu *Cumulonimbus*. Wanahewa (*Meteorologists*) wamechunguza ni namna gani mawingu ya mvua cumulonimbus hujitengeneza na ni namna gani yanatengeneza mvua, mvua ya mawe na, mmeto wa radi.

Wamegundua kuwa mawingu ya cumulonimbus yanapitia hatua zifuatazo ili kuzalisha mvua:

1) **Mawingu husukumwa na upepo:** Mawingu ya Cumulonimbus yanaanza kujiunda pale upepo unaposukuma baadhi ya vipande vidogo vidogo vya mawingu (cumulus clouds) kuelekea katika sehemu, yanapokutania. (tazama umbo 17 na 18).





***Umbo 17:** Picha ya Satellite inaonyesha mwendo wa mawingu kuelekea sehemu za kukutania zenye alama ya B,C, na D. Mishale inaashiria muelekeo wa upepo. (Matumizi ya picha za satellite kwa ajili ya uchambuzi na utabiri wa hali ya hewa, Anderson and others, ukurasa wa, 188).*



***Umbo 18:** Vipande vidogo vidogo vya mawingu (cumulus clouds) vikielekea sehemu ya mkusanyiko karibu na horizon,[1] ambapo tunaweza kuona wingu kubwa la cumulonimbus. (Clouds and Storms, Ludlam plate 7.4.)*

[1] Mstari wa upeo wa macho.

2) **Kuungana:** Kisha yale mawingu madogo madogo huungana pamoja na kutengeneza wingu kubwa[1] (tazama umbo 18 na 19).





*Umbo 19: (A) vipande vidogo vidogo vya mawingu vilivyojitenga (cumulus clouds). (B) Wakati mawingu madogo madogo yanapoungana pamoja, yanajirundika na wingu kubwa linaongezeka, kwahiyo wingu limesharundikana. Matone ya mvua yanayodondoka yanaonyeshwa kwa alama ya • (The Atmosphere, Anthes and others, ukurasa wa, 269.)*

**3) Mrundikano:** Wakati mawingu madogo madogo yanapoungana pamoja, yanapanda ndani ya wingu kubwa kwa nguvu za mikondo ya upepo inayoelekea juu. Mnyanyuko kuelekea juu kwa msukumo wa upepo, katika sehemu za karibu na katikati ya wingu una nguvu zaidi kuliko sehemu za pembeni[2]. Mikondo hiyo ya hewa inayopanda juu husababisha umbo la wingu linyooke kiwima kiwima, kwahiyo wingu linakuwa limejirundika pamoja (tazama umbo 19 (B), 20, na 21). Ukuaji huu wa kiwima wima unasababisha umbo la wingu kutawanyika katika sehemu za anga zenye baridi, ambazo hujiunda na kuwa matone ya maji na vipande vya barafu (mvua ya mawe) na yanaanza kukua makubwa zaidi. Wakati matone

---

[1] Tazama The Atmosphire, Anthes and others
pp. 268-269, and Elements of Meteorogy, Miller and Thampson, p. 141.
[2] Maeneo ya karibu na katikati mwa wingu yanakuwa imara zaidi, hii inatokana na sehemu hii kulindwa na mawingu yaliyo zunguka pambizoni mwake

haya ya maji na vipande vya barafu vinapokuwa vizito kupita kiasi na kushindwa kusukumwa (kubebwa) na mikondo ya upepo,[1] yanaanza kudondoka chini kutoka mawinguni, yakiwa kama ndio mvua, barafu n.k.[2].




***Umbo 20:** Wingu la mvua Cumulonimbus. Baada ya wingu hilo kurundikana pamoja, tayari mvua inaanza kunyesha kutoka kwenye wingu hilo. (Weather and Climate, Bodin, ukurasa wa, 123.)*

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴾Je! Huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu huyasukuma mawingu, kisha huyaambatisha, kisha huyafanya mirundi? Basi utaona mvua ikitoka kati yake....﴿ Qur'an, 24:43**



***Umbo 21:** Wingu la mvua Cumulonimbus. (A Colour Guide to Clouds, Scorer and Wexler, ukurasa wa, 23.)*

---

[1] Hewa ya gesi yenye nguvu kama umeme ambayo inayasukuma mawingu haya ya mvua lakini asili yake ni upepo

[2] Angalia kitabu: *The Atmosphere*,cha Anthes and others, ukurasa wa, 269, na kitabu: *Elements of Meteorology*, Miller and Thompson

Wataalamu wa hali ya hewa, nyota, na vimondo ni hivi karibuni tu wamefahamu kwa undani habari hizi, za muundo wa mawingu, umbo na shughuli zake, kwa kutumia vyombo vilivyoendelea vyenye uwezo wa hali ya juu, kama vile ndege, satelaiti kompyuta, mabaluuni (maputo makubwa), na baadhi ya nyenzo nyenginezo, zitumikazo kuchunguza upepo na muelekeo wake, ili kupima unyevunyevu na aina zake, na kupambanua viwango vya msukumo wa hewa na mabadiliko yake[1].

Aya iliyotangulia, baada ya kuelezea mawingu na mvua, inaeongealea barafu (matone manene ya mvua kama mawe) na mimeto ya radi:

> **❮....Na huteremsha kutoka juu kwenye milima ya mawingu mvua ya mawe, akamsibu nayo amtakaye na akamuepusha nayo amtakaye. Hukurubia mmetuko wa umeme wake kupofua macho❯** Qur'an, 24:43

Wataalamu wa hali ya hewa, wamegundua kuwa mawingu haya ya mvua cumulonimbus, ambayo ndiyo yanayoshusha mvua ya mawe (matone manene ya mvua kama mawe) yanafikia muinuko wa[2] urefu wa futi 25,000 hadi 30,000. (ambayo ni sawa na maili 4.7 hadi 5.7)[3] urefu ambao ni sawa na urefu wa milima, kama ilivyosema Qur'an: (...Na huteremsha kutoka juu kwenye milima ya mawingu mvua ya mawe...) (angalia umbo namba 21)


---

[1] Angalia kitabu: *Ee'jaz al-Qur'an al-kareem fee Wasf Anwa' al-Riyah, al-Sohob, al-Matar,* Makky and others, ukurasa wa, 55

[2] Mvua ya mawe ni mvua ya baridi kali iangushayo vipande vya barafu vilivyo vigumu sana kama mawe

[3] *Elements of Meteorology*, Miller and Thompson, ukurasa wa, 141.

Aya hii inaweza kuibua swali. Kwanini aya imesema "mmetuko wa umeme wake ? " ilipokuwa ikiongelea kuhusu barafu (mvua ya mawe)? Je hii ina maana kwamba barafu ya mvua ya mawe ndio muhusika mkuu wa kuzalisha mmetuko wa radi? Hebu tutazame kinasema nini kitabu kiitwacho *Meteorology Today* kuhusu swala hii. Kinasema kwamba mawingu yanakuwa yamejaa umeme pale madonge ya barafu yanapoanguka kupitia katika mawingu yenye matone ya baridi mno na yenye madonge ya barafu. Wakati matone ya maji ya sehemu hii yanapogongana na matone ya barafu, yanaganda kwa kule kugusana na hutoa joto lililojificha (la ndani kwa ndani).[1] Hali hii inapelekea upande wa nje wa vipande vya matone ya barafu kuwa na moto zaidi kuliko vile vipande vilivyokaribu na madonge ya barafu. Wakati matone ya barafu yanapokutana na donge la barafu, kunatokea tukio muhimu sana la aina yake: umeme hutiririka kutoka katika vipande vyenye baridi zaidi kuelekea vipande vyenye joto zaidi. Kulingana na hali hiyo vipande vya mawe ya barafu vinakuwa vina chaji hasi (-) Na athari hiyo hiyo hutokea wakati matone yenye baridi mno, yanapokutana na kipande cha jiwe la barafu na hapo hutokea vipunjepunje vidogo vidogo sana vya chanya (+) ambavyo huyeyuka. na hivi vipunje punje vyepesi vya chanya, baadae husombwa na mikondo ya upepo[2] inayopanda na kupelekwa sehemu ya juu ya wingu. Na vile vipande vya barafu vilivyosalia na chaji hasi (-) vinadondoka kuelekea chini ya wingu,



[1] Mvuke wa moto wa kiasi hali ya kuwa joto joto
[2] Upepo wenye hewa au nguvu kama gesi

kwa hiyo sehemu ya chini kabisa ya wingu inakuwa ina chaji hasi (-) Na hizi chaji hasi baadae zinalipuka zikiwa ndio mmetuko wa umeme.[1] Kutokana na haya tunakamilisha kuwa barafu ndio mhusika mkuu wa uzalishaji wa mmeto wa umeme wa radi.

Maelezo haya juu ya mmetuko wa umeme wa radi yamegundulika hivi karibuni. Kwani mpaka kufikia mwaka 1600 AD, fikira za Aristotle kuhusu hali ya hewa ndizo zilizokuwa zimetawala. Kwa mfano, Aristotle alisema ya kwamba tabaka za anga zina aina mbili za hewa nyevunyevu na kavu. Pia amesema kuwa radi ni sauti itokanayo na mgongano wa hali ya hewa yabisi na mawingu yaliyo karibu, na mmetuko ni muwako na muunguo wa hewa kavu ukiwa na umbo la moto mwembamba uliofifia.[2] Hizi ni baadhi ya fikira juu ya hali ya hewa, ambazo zilikuwa zimetawala katika kipindi cha kushuka Qur'an, karne kumi na nne zilizopita.

## H) Maelezo ya Wanasayansi juu ya Miujiza ya kisayansi ndani ya Qur'an

Yafuatayo ni baadhi ya maelezo ya wanasayansi juu ya miujiza ya kisayansi iliyomo ndani ya Qur'an tukufu. Maelezo yote haya yamechukuliwa toka kwenye mkanda wa video uitwao *This is the truth.* (Huu ndio ukweli). Katika mkanda huo wa video unaweza kuwaona na kuwasikia wanasayansi wakitoa maelezo yafuatayo: (Tafadhali tembelea www.islam-guide.com/truth ili kujipatia nakala ya mkanda huu, na kujionea mkanda huo moja kwa moja, au kujionea picha za video za maelezo hayo moja kwa moja.

1) Dr. T. V. N. Persaud ni Professor wa elimu ya uchanganuzi wa mwili na viungo vyake (anatomia), Professor wa tiba za watoto na ni Professor wa ukunga, elimu ya uzazi na sayansi ya kuzaliana

---

[1] Meteorology Today, Ahrens, p. 437.

[2] *The works of Aristotle Translated into English: Meteorologica*, Vol. 3, Ross and others, ukurasa wa, 369a- 369b.

katika chuo kikuu cha Manitoba, Canada. Na huko chuoni, alikuwa ni Mwenyekiti wa kitivo cha Anatomia kwa muda wa miaka 16. naye ni mtu mashuhuri sana katika sekta yake. Naye ni mtunzi wa vitabu 22 vya kiada na ameshachapisha zaidi ya miswada 181 ya kisayansi. Mwaka 1991 alitunukiwa tunzo nzuri sana itolewayo kwa ajili ya sekta ya Anatomia nchini Canada ambayo ni zawadi kuu maalum ya J.C.B. inayotolewa na umoja wa wataalamu wa Anatomia wa kikanada. Alipoulizwa kuhusu miujiza ya kisanyasi iliyomo ndani ya Qur'an, ambayo ameshaichunguza, alieleza yafuatayo:

Kwa njia ambayo nilielezwa ni kuwa Muhammad alikuwa ni mtu wa kawaida. Hakujua kusoma wala kuandika. Kwa hakika Muhammad alikua hajui kusoma na kuandika. Nasi tunaongelea kuhusu karne kumi na mbili, kwa hakika ni kumi na nne zilizopita. Una mtu asiejua kusoma wala kuandika anatangaza na anatoa maelezo, na maelezo hayo ni fasaha na yakustajabisha kuhusu tabia ya kisayansi. Na mimi binafsi sidhani kuwa mambo yote haya yametokea kibahati bahati tu. Kuna mambo mengi sana ya hakika na kama alivyo Dr. Moore, sina pingamizi yeyote katika akili yangu ya kuwa huu ni wahyi au ufunuo mtakatifu toka kwa Mungu uliomuongoza kuweza kutoa maelezo haya.

Professor Persaud ameambatanisha baadhi ya aya za Qur'an na hadithi za mtume Muhammad ﷺ katika baadhi ya vitabu vyake. Pia alionyesha aya hizi na hadithi za mtume Muhammad ﷺ katika mikutano kadhaa.

2) Dr. Joe Leigh Simpson ni Mwenyekiti wa kitivo cha ukunga, na uzazi, Professor wa ukunga na uzazi, na ni Professor wa elimu ya viini vinavyorithiwa toka kwa wazazi na elimu ya viini vya binadamu (Genetics) katika chuo cha mafunzo ya tiba cha Houston Texas nchini Marekani. Zamani alikuwa ni Professor wa magonjwa ya wanawake na ukunga (Ob-Gym) na ni mwenyekiti wa kitivo cha magonjwa ya wanawake na ukunga katika chuo kikuu cha

Tennessee, Memphis, University of Tennessee, Memphis, Tennessee, USA. Pia aliwahi kuwa rais wa umoja wa watungishaji mimba (warutubishaji Fertility) wa Marekani. Ameshawahi kutunukiwa tunzo nyingi ikiwemo ile iliyotolewa mwaka 1992 na chama cha maprofesa wa utambuzi wa maradhi ya wanawake na ukunga. Professor Simpson alizichunguza hadithi mbili za mtume Muhammad zifuatazo:

**{Hakika kila mmoja wenu, hukusanywa pamoja umbo lake akiwa tumboni mwa mama yake katika muda wa siku arobaini.....}**[1]

**{Zikipita siku arobaini na mbili kwa tone la manii (lililo tumboni mwa mama yake) Mwenyezi Mungu analipelekea malaika kwenda kulitia umbo, kutengeneza usikivu wake, uoni wake, ngozi yake, nyama zake, na mifupa yake....}**[2]

Alizichunguza hadithi hizi mbili za mtume Muhammad ﷺ kwa upana, akaweka maanani kuwa siku arobaini za kwanza ndizo zifanyazo hatua ya kipekee na iliowazi ya mwanzo wa mimba (kiinitete). Na alivutiwa hasa na usahihi mkamilifu pomoja na uangalifu barabara wa hadithi hizi za mtume Muhammad ﷺ. Kisha, alipokuwa katika moja ya mikutano, alitoa rai ifuatayo:

---

[1] Angalia kitabu: *Saheeh Muslim*, #2643, na *Saheeh Al-Bukhari*, #3208. Zingatia: Maelezo yaliyo katikati ya mabano ya aina hii {....} katika kitabu hiki ni tafsiri ya kile alichokisema Mtume Muhammad ﷺ. Pia zingatia kuwa alama hii # ikitumika katika footnotes, inaashiria namba ya hadithi. Hadithi ni nukuu ya uhakika iliyoelezwa na wafuasi wa Mtume Muhammad ﷺ juu ya kile alichokisema, tenda, au alichokikiri.

[2] *Saheeh Muslim*. #2645.

"Kwa hiyo hadithi hizi mbili (maneno ya mtume Muhamadﷺ) zilizonukuliwa zimetupatia ratiba maalumu ya hatua za msingi za maendeleo ya ukuaji wa mimba kabla ya siku arobaini. Pia, kitu cha muhimu kimeshawekwa, nafikiri tayari imesharudiwa rudiwa na wazungumzaji wengine asubuhi hii: haiwezekani kuwa hadithi hizi zimepatikana kutokana na misingi ya elimu za sayansi zilizokuwepo wakati zilipoandikwa hadithi hizi..... Kinachofuata, nadhani, ni kwamba, sio tu hakuna kupingana kati ya elimu ya chembe chembe hai (Genetics) na dini lakini, kwa hakika, dini inaweza kutoa muongozo kwa sayansi kwa kuongeza wahyi (ufunuo) katika baadhi ya mitazamo ya kimapokeo (traditional) ya kisayansi, kwani kuna maelezo katika Qur'an yaliyotayari, yametajwa tangu karne nyingi, zilizopita na bado ni thabiti yanayothibitisha kuwa elimu iliyomo ndani ya Qur'an imetoka kwa Mwenyezi Mungu."

3) Dr. E. Marshall Johnson ni Profesa wa heshima (aliestaafu) wa elimu ya anatomia na maendeleo ya kibaiolojia katika chuo kikuu cha Thomas Jefferson, Philadelphia, Pennsylvania, USA. Ambako kwa muda wa miaka 22 alikuwa ni Profesa wa anatomia, mwenyekiti wa kitengo cha anatomia, na Mkurugenzi wa chuo cha Daniel Baugh, Daniel Baugh Institute. Vilevile alikuwa rais wa chama cha wachunguzi wa maajabu ya viumbe (Teratology Society), Dr. Johnson ameshatunga zaidi ya nyaraka 200. Mnamo mwaka 1981, katika mkutano wa saba wa utabibu uliofanyika Dammam, Saudi Arabia, Profesa Johnson alipokuwa akiwasilisha nyaraka zake za uchunguzi alisema:

"Kwa ufupi: Qur'an sio tu inafafanua maendeleo ya mfumo wa nje, lakini pia inasistizia hatu za ndani, hatua zilizo ndani ya kiinitete (mimba), hatua za uumbwaji na ukuaji, inasistizia matukio makuu yanayotambulika na sayansi ya kisasa."

Vile vile amesema: "Nikiwa kama mwanasayansi, ninaweza kushughulika na vitu ambavyo ninaviona dhahiri tu. Naweza

kufahamu utungo wa mimba na ukuaji wa kibailojia. Naweza kufahamu matamko niliyotafsiriwa kutoka katika Qur'an. Kama nilivyotangulia kutoa mfano hapo mwanzo, kama ingenilazimu kuhamia zama zile zilizoshushwa Qur'an, na nikajua yale ninayoyajua leo na kuchambua vitu, nisingeweza kutoa maelezo ya vitu, vilivyo elezwa ndani ya Qur'an. Sioni ushahidi wowote wa kukanusha kuwa Muhammad, kapata maelezo haya toka sehemu fulani. Kwa hiyo sioni chochote kinachopingana na ufahamu wa kuwa ufunuo mtakatifu umehusika katika kile alichoweza kukiandika Muhammad[1].

4) Dr. William W. Hay ni mwanasayansi mashuhuri katika utaalamu wa mambo ya bahari. Yeye ni Profesa wa sayansi ya jiolojia katika chuo kikuu cha Colorado, University of Colorado, Boulder, Colorado, USA. Alikuwa mkuu wa zamani wa shule ya Rosenstiel ya mambo ya bahari na sayansi ya hali ya hewa, katika chuo kikuu cha Miami, Florida, USA. Baada ya mjadala na Profesa Hay juu ya mambo ya hakika yaliotajwa na Qur'an kuhusiana na bahari mambo ambayo yamegunduliwa hivi karibuni, amesema:

"Naona kuwa ni jambo la kusisimua mno kuona kuwa maelezo ya aina hii yapo katika maandiko ya kale ya Qur'an tukufu, na sina jinsi ya kufahamu yametoka wapi maandiko hayo, ispokuwa nafikiri ni jambo la kuvutia mno kuwa maandiko hayo yapo katika kitabu hicho na kuwa kazi hii inaendelea kwa ajili ya kugundua maelezo hayo, nayo ni maana ya baadhi za ibara." Na pale alipoulizwa, kuhusiana na chanzo cha Qur'an, alijibu:

"Vizuri, nadhani kuwa chanzo chake lazima kitakuwa ni Mungu"

---

[1] Mtume Muhammad ﷺ alikuwa hajui kusoma na kuandika. Lakini aliwasomea hio Qur'an Maswahaba zake na aliwaamuru baadhi ya maswahaba hao waiandike.

5) Dr. Gerald C. Goeringer ni mhadhiri na ni Profesa mshiriki wa tiba ya uzazi na mimba katika kitengo cha baiolojia ya seli, shule ya uganga, chuo kikuu cha Georgetown, University, Mjini Washington, DC, USA. Katika mkutano wa nane wa kitabibu uliofanyika mjini Riyadh, Saudi Arabia, Profesa Goeringer alitoa maelezo yafuatayo wakati anawasilisha nyaraka zake za uchunguzi:

"Kwa kiasi fulani aya chache (aya za Qur'an) zimekusanya maelezo kwa upana yanayohusiana na ukuaji wa binadamu tangu wakati wa mchanganyikano wa mbegu (Seli pevu za uzazi) kupitia (organogenesis). Hakuna sifa za kipekee kama hizo wala rekodi kamili za ukuajia wa binadamu, kama vile uainishaji, istilahi, na ufafanuzi, zilizokuwepo hapo kabla. Na mara nyingi, kama si zote, mathalani, maelezo haya yametangulia kwa karne nyingi kushinda rekodi zote zinazotunza hatua mbalimbali za mimba ya binadamu na rekodi za ukuaji wa kijusi (kidudu cha manii) rekodi zilizo katika maandiko ya zamani ya kisayansi."

6) Dr. Yoshihide Kozai ni profesa wa heshima (aliestaafu) katika chuo kikuu cha Tokyo University, Hongo, Tokyo, Japan, Na alikuwa mkurugenzi wa kituo cha taifa cha uchunguzi wa hali ya anga cha Japani, katika mji wa Mitaka, Tokyo, Japan, amesema:

"Nimevutiwa sana kwa kukuta ukweli na uhakika wa mambo ya anga ndani ya Qur'an, na sisi, wanaanga wa kisasa tumejifunza sehemu ndogo tu za ulimwengu. Katika juhudi zetu tumezingatia sana juu ya sehemu ndogo sana ya ulimwengu. Na hii ni kwa sababu, kwa kutumia darubini, tunaweza kuona sehemu ndogo tu ya mbingu bila kufikiri kuhusu ulimwengu mzima. Kwa hivyo kutokana na kusoma Qur'an na kujibu maswali, nafikiri naweza kupata njia yangu ya badae (mustaqbali, future) itakayoniwezesha kuchunguza ulimwengu.

7) Profesa Tejatat Tejasen ni mwenyekiti wa kitengo cha Anatomia katika chuo kikuu cha Chiang Mai, nchini Thailand.

Zamani, alikuwa ni mkuu wa kitivo cha udakitari katika chuo kikuu hicho hicho. Katika kipindi cha mkutano wa nane wa kitabibu ulio fanyika Riyadh, nchini Saudi Arabia, profesa Tejasen alisimama na kusema:

"Katika kipindi cha miaka mitatu, nimekuwa navutiwa na Qur'an .... Kutokana na uchunguzi wangu na kile nilichojifunza kutoka katika mkutano huu, naamini kuwa kila kitu kilichosajiliwa ndani ya Qur'an kwa karne kumi na nne zilizopita lazima kitakuwa ni kitu cha kweli, ambacho kinaweza kuthibitishwa na vigezo vya kisayansi. Na kutokana na kuwa mtume Muhammad ﷺ alikuwa hajui kusoma wala kuandika, Muhammad lazima atakuwa ni mjumbe (wa Mungu), ambae ndie alieuleta ukweli huu, ambao ulifunuliwa kwake ukiwa kama mwangaza kutoka kwa anaestahiki peke yake kuwa ni Muumba. Muumbaji huyu lazima atakuwa ni Mungu. Kwa hivyo, nafikiri huu ni wakati muafaka wakusema *La ilaha illa Allah*, Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ispokuwa Allah, *Muhammadur rasoolu Allah,* Muhammad ni Mtume wa Mungu. Mwisho ni wajibu wangu kutoa pongeza kwa haya maandalizi yenye mafanikio ya hali ya juu kuhusiana na mkutano huu...... nimepata faida, sio tu kutokana na mtazamo wa kisayansi na mtazamo wa dini, lakini pia nimefaidika kwa kupata nafasi tukufu ya kukutana na wanasayansi wengi mashuhuri na nimepata marafiki wengi wapya miongoni mwa washiriki katika mkutano huu. Kitu cha thamani sana katika hivyo, nilichokipata kwa kuja kwangu katika sehemu hii ni *La ilaha illa Allah, Muhammadur rasoolu Allah,* na kuwa nimekuwa muislamuu."

Baada ya mifano yote hii tuliyoiona kuhususiana na miujiza ya kisayansi iliyomo ndani ya Qur'an na baada ya maelezo yote ya wanasayansi juu ya jambo hili, hebu wacha tujiulize maswali haya:

► Je inawezekana kuwa ni bahati tu kuwa maelezo yote haya ya ugunduzi wa kisasa wa kisayansi kutoka katika sekta mbali mbali

yaliyotajwa ndani ya Qur'an, ambayo imeshushwa tangu karne kumi na nne zilizopita?
► Je inawezenaka kuwa hii Qur'an imetungwa na Muhammad au mtu mwengine yeyote?

Jibu pekee linaloweza kupatikana ni kwamba Qur'an lazima itakuwa ni maneno halisi ya Mwenyezi Mungu, yaliyofunuliwa nae (Mwenyezi Mungu ).

(Kwa maelezo zaidi, makala za moja kwa moja, vitabu, au kanda za video za miujiza ya kisayansi ndani ya Qur'an, takatifu, Tafadhali tembelea www.islam-guide.com/science au wasiliana na moja ya Jumuiya zilizoorodheshwa katika ukurasa wa, 69.)

## (2) Changamoto Kuu ya Kuunda Sura Moja kama Sura za Qur'an Tukufu

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴾Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake, na muwaite mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli. Na mkitofanya - na wala hamtofanya kamwe - basi uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe walio andaliwa hao wanao kanusha. Na wabashirie walio amini na wakatenda mema kwamba watapata mabustani yapitayo mito kati yake....﴿ Qur'an, 2:23-25**

Tangu kushushwa Qur'an, karne kumi na nne zilizopita, hakuna mtu hata mmoja aliyeweza kutunga sura moja tu iliyo mfano wa Sura za Qur'an kiuzuri, kiumbuji (ufasaha na ushawishi), kiutamu

wa maneno, sheria za kihekima, maelezo ya kweli, utabiri wa kweli, na sifa nyenginezo za ukamilifu. Pia zingatia kuwa, sura iliyo ndogo kabisa katika Qur'an ni (Sura ya 108) ambayo ina jumla ya maneno kumi tu, Lakini pamoja na hivyo hakuna kiumbe yeyote aliyeweza kuifikia changamoto hii, tangu enzi hizo mpaka leo[1]. Baadhi ya Wapagani[2] wa kiarabu ambao walikuwa ni maadui wa Muhammad ﷺ walijaribu kutaka kuifikia changamoto hii ili kutaka kuthibitisha kuwa Muhammad si Nabii wa kweli, lakini walishindwa kutekeleza jambo hilo.[3] Kushindwa huko kulitokea ingawa ni kweli kwamba Qur'an ilishushwa kwa lugha na lahaja yao na kwamba Warabu wa wakati huo wa Muhammad ﷺ walikuwa ni wnaumbuji hodari (lugha ya kushawishi ufasaha-balagha) ambao walitunga mashairi mazuri na yenye ubora wa hali ya juu ambayo yanaendelea kusomwa na kuthaminiwa mpaka leo hii. Sura ya 108 ambayo ndio sura ndogo kabisa katika Qur'an, yenye Maneno kumi tu, Lakini mpaka sasa hakuna hata mtu mmoja aliyeweza kuifikia hiyo changamoto ya kutunga sura moja iliyo kama sura za Qur'an.

*Sura iliyo ndogo zaidi katika Qur'an (Sura 108) ina jumla ya maneno kumi, Lakini mpaka sasa hakuna hata mtu mmoja aliyeweza kuifikia hiyo changamoto ya kutunga sura moja iliyo kama sura za Qur'an.*





---

[1] Angalia: Al-Borhan fee Oloom Al-Qur'an, Al-Zarkashy, kitabu cha pili, ukurasa wa, 224.

[2] Wapagani ni watu wa aina yeyote wanaoabudu Masanamu, Jua, Mwezi, Moto, au kitu chchote kwa imani ya kuwa ni mungu, wakati huohuo wanakiri kuwa kuna Mungu wa kweli (Allah).

[3] Angalia: Al-Borhan fee Oloom Al-Qur'an, Al-Zarkashy, kitabu cha pili, ukurasa wa, 226.

# (3) Utabiri wa Biblia juu ya kuja kwa Muhammad ﷺ, Mtume wa Uislamu




Utabiri wa Biblia juu ya kuja kwa Mtume Muhammad ﷺ ni uthibitisho juu ya ukweli wa Uislamu kwa watu wanaoamini Biblia.

Katika kumbukumbu ya torati 18, Musa ameeleza kuwa Mungu amemwambia:

> **"Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, na nitatia maneno yangu kinywani mwake, nae atawaambia yote nitakayo mwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyesikililiza maneno yangu atajayo sema yule kwa jina langu, nilitaka kwake." kumbukumbu ya torati 18-19**

Kutokana na aya hizi tunahitimisha kwa kusema kuwa Nabii aliyetajwa ndani ya utabiri huu lazima atakuwa na sifa tatu zifuatazo:

1) Ya kwamba atukuwa anafanana na Musa.
2) Ya kwamba atakuwa ni miongoni mwa ndugu wa waizraeli, yaani atatokea ukoo wa Ismaili.
3) Ya kwamba Mwenyezi Mungu ataweka Maneno yake kwenye kinywa cha Mtume huyu na kwa hivyo basi atatangaza kile ambacho Mungu amemuamuru.

Wacha tuzichunguze kwa undani zaidi sifa tatu hizi.

## 1) Nabii kama Musa:

Hakukuwa na Manabii wawili waliokuwa wakifanana sana kama Musa na Muhammad ﷺ. Wote wawili walipewa sheria na kanuni za maisha zilizokamilika. Wote walikabiliana na maadui zao na wakawashinda kwa njia za kimiujiza. Wote wawili walikubaliwa kuwa ni Mitume na ni Watawala wa nchi zao. Wote waliihama miji yao kufuatana na njama za kuwaua. Mlingano kati ya Musa na Yesu (Isa) hauafikiani sio tu kwa sifa za kufanana zilizotajwa hapo juu lakini pia kwa sifa nyinginezo muhimu sana. Na miongoni mwa sifa hizo ni kuzaliwa kwa njia za kikawaida, maisha ya kifamilia, na kifo cha Musa na Muhammad ﷺ lakini hayo hayapo kwa Yesu (Isa). Na zaidi ya hayo Yesu alizingatiwa na wafuasi wake kuwa ni Mwana wa Mungu na si mtume wa Mungu tu, kama walivyokuwa Musa na Muhammad ﷺ na kama waisilamu wanavyoamini kuwa hivyo ndivyo alivyokuwa Yesu. Kwa hiyo, utabiri huu unaelekezwa kwa Muhammad ﷺ na sio kwa Yesu, kwa sababu Muhammad ﷺ ndiye anayefanana zaidi na Musa kuliko Yesu.

Vile vile mojawapo ya maandiko katika Injili ya Yohana yanaeleza kuwa Mayahudi walikuwa wakisubiri ukamilisho wa kuja manabii watatu tofauti: 1) kuja kwa Kristo (Yesu), 2) kuja kwa Eliyah, 3) kuja kwa Nabii. Maelezo haya yapowazi kutokana na maswali matatu aliyoulizwa Yohana mbatizaji**:**

> "Viongozi wa Wayahudi waliwatuma makuhani na Walawi wakamwulize Yohana, ``Wewe ni nani?" 20Yohana akawajibu wazi wazi pasipo kuficha, ``Mimi siye Kristo." 21Wakamwuliza, ``Wewe ni nani basi? Wewe ni Eliya ?" Akajibu, ``Hapana, mimi siye." ``Wewe ni yule Nabii?" Akajibu, ``Hapana." **Yohana 1:19-20**

Kama tutaangalia katika Biblia pamoja na marejeo, katika noti za pambizoni sehemu ambayo neno “Prophet-nabii” lilitokea katika Yohana 1:21, tutakuta kuwa maneno hayo yanaashiria utabiri wa Kumbukumbu ya torati 18:15 na 18:18.[1] Kutokana na hayo tunakamilisha kuwa Yesu Kristo sio mtume alietajwa katika kumbukumbu ya torati 18:18.

**2) Ni miongoni mwa ndugu wa waizraeli:**

Ibrahim alikuwa na watoto wawili, Ismaili na Isaka (Mwanzo 21). Ismaili akawa babu wa taifa la Waarabu, na Isaka akawa babu wa taifa la Wayahudi. Nabii aliyeelezwa hakuwa ni mwenyekuja kutokea miongoni mwa Wayahudi wenyewe, lakini atatokea miongoni mwa ndugu zao yaani kizazi cha Ismaili. Muhammad ﷺ, ambae ni mjukuu wa Ismaili, bila shaka ndie huyo Nabii alietabiriwa.

Villevile Isaya 42:1-13. inazungumzia kuhusu mtumishi wa Mungu, “Mteule” wake na ni “Nabii” atakaeleta Sheria. **"Hata zimia wala hata kata tamaa, hata atakapoweka hukumu duniani; na visiwa vitaingojea sheria yake." Isaya 42:4**

Aya ya 11 inafungamana na Nabii mtarajiwa kutoka kizazi cha Kedar. Kedar ni nani? Kulingana na maelezo ya Mwanzo **25:13,** Kedar alikuwa ni mtoto wa pili wa Ismaili, Kader alikuwa ni mhenga (babu) wa Mtume Muhammad ﷺ.

**3) Mwenyezi Mungu ataweka Maneno yake katika kinywa cha Nabii huyu:**

Maneno ya Mwenyezi Mungu (Qur'an takatifu) kwa kweli yaliwekwa katika kinywa cha Nabii Muhammad ﷺ. Mwenyezi

---

[1] Tazama notes za pambizoni katika The NIV Study Bible, New International Version on verse 1:21, p. 1594.

Mungu alimtuma Malaika Jibrili (Gabriel) kwenda kumfundisha Muhammad ﷺ, Maneno asilia ya Mwenyezi Mungu (Qur'an Takatifu) na alimuamuru Muhammad awasomee watu maneno hayo kama alivyoyasikia. Kwa hiyo hayo maneno si maneno ya Muhammad. Hayo maneno hayakuja kutoka kwenye fikra zake binafsi, lakini yaliwekwa katika kinywa chake kupitia Malaika Jibrili. Katika kipindi cha uhai wa Muhammad ﷺ na chini ya usimamizi wake, wafuasi wake waliyahifadhi na kuyaandika maneno hayo.

> Zingatia kwamba Mungu amesema katika utabiri wa kumbukumbu ya torati: **"hata itakuwa mtu asiye sikiliza maneno yangu atajayosema yule kwa jina langu nilitaka kwake." kumbukumbu ya Torati 18:19**

"*If anyone does not listen to my words that the prophet speaks in my name, I myself will call him to account.”* **(*Deuteronomy, 18:19*)** Hii ikiwa na maana kuwa mtu yeyote anaeamini Biblia anapaswa kuamini kinachosemwa na Nabii huyo, na Nabii huyo ni Muhammad ﷺ.

(Kwa maelezo zaidi kuhusu Muhammad ﷺ ndani ya Biblia tafadhali tembelea www.islam-guide.com/mib ).

# (4) Aya za Qur'an Ambazo zimeeleza kutokea Matukio katika Siku za mbele na Kisha Yakatokea

Mfano wa matukio yaliyo tabiriwa katika Qur’an ni ushindi wa Warumi dhidi ya Wafursi ndani ya kipindi cha miaka mitatu hadi

tisa baada ya Warumi kushindwa vibaya na Wafursi. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴿Warumi wameshindwa, Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda, Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi﴾ Qur'an, 30:2-4**

Hebu acha tuone historia inatuambia nini kuhusu vita hivyo. Kitabu kiitwacho *History of the Byzantine State* kinasema kuwa jeshi la Warumi lilishindwa vibaya sana katika eneo la Antokia (Antioch) mnamo mwaka 613, na matokeo yake Wafursi walisonga mbele kidogo kidogo kila upande[1]. Kwa wakati huo ilikuwa ni vigumu kufikiria kuwa Warumi wangeweza kuja kuwashinda Wafursi, lakini Qur'an ilitabiri kuwa Warumi watakuwa Washindi, ndani ya kipindi cha miaka mitatu hadi tisa. Na mnamo mwaka 622, ikiwa ni miaka tisa tangu kushindwa kwa Warumi, Majeshi hayo mawili (Warumi na Wafursi) yalikutana katika viwanja vya Armenia, na matokeo yalikuwa ni ushindi mkubwa wa Warumi dhidi ya Wafursi, na hiyo ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu kushindwa kwa Warumi mnamo mwaka 613.[2] Utabiri ulikamilika, kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika Qur'an.

Vilevile zipo aya nyingi ndani ya Qur'an na Hadithi za Muhammad ﷺ. ambazo zinataja matukio ya siku za mbele ambayo baadae yakatokea.

---

[1] History of the Byzantine State, Ostrogorsky, ukurasa wa, 95

[2] History of the Byzantine State, Ostrogorsky, ukurasa wa, 100-101 Na pia katika kitabu: History of Persia, Sykes, Vol. 1, ukurasa wa, 483-484. Vilevile angalia kitabu: The New Encyclopaedia Britannica, Micropaedia Vol. 4, ukurasa wa, 1036.

# (5) Miujiza iliyofanywa na Mtume Muhammad ﷺ

Miujiza mingi ilifanywa na Mtume Muhammad ﷺ kwa ruhusa ya Mungu. Miujiza hiyo ilishuhudiwa na watu wengi. Kwa mfano:

- Pale makafiri wa Makka walipomtaka Mtume Muhammad ﷺ awaonyeshe miuujiza, akawaonyesha muujiza wa kupasuka kwa Mwezi.[1]

- Muujiza mwingine ulikuwa ni kububujika maji kutoka katika vidole vya Muhammad ﷺ. Pale wafuasi wake walipopatwa na kiu na walikuwa hawana maji ispokuwa maji kidogo yaliyokuwepo katika chombo. Walimuendea Mtume na wakamwambia ya kuwa hawana maji ya kutawadha wala ya kunywa ispokuwa yale yaliyokuwa katika chombo. Kwa hiyo, Muhammad ﷺ. aliingiza Mkono wake katika kile chombo, na maji yakaanza kububujika kutoka katikati ya vidole vyake. Kwa hivyo wakanywa na kutawadha. Idadi yao ilikuwa ni wafuasi elfu moja na miatano.[2]

Vilevile kulikuwa na miujiza mingine mingi ambayo ilifanywa na Mtume au iliyomtokea.

# (6) Maisha ya hali ya chini ya Muhammad ﷺ

Kama tutalinganisha maisha ya Muhammad kabla ya kupewa ujumbe akiwa ni mtume na maisha yake baada ya kuanza kutekeleza kazi ya utume, Tutahimisha kuwa haingii akilini kudhani kuwa

[1] Saheeh Al-Bukhari, #3637, na Saheeh Muslim, #2802
[2] Kitabu: Saheeh Al-Bukhari, #3576, na Saheeh Muslim, #1856.

Muhammad ﷺ alikuwa ni mtume wa uongo, ambae amedai utume ili achume mali, ukubwa, utukufu, au nguvu.

Kabla ya kazi yake ya utume hakuwa na matatizo yoyote ya kiuchumi. Akiwa ni mfanyabiashara mashuhuri na aliefanikiwa, Muhammad ﷺ alijihakikishia kujitosheleza na pato la kufarijisha. Baada ya kupewa kazi ya utume na kwasababu ya utume huo, akawa na hali ngumu kiuchumi. Ili kubainisha hayo kwa uwazi zaidi, acha, tupitie kauli zifuatazo zinazohusiana na maisha yake:

- **Aisha, ambaye alikuwa ni mke wa Muhammad ﷺ, amesema: "Oo mtoto wa kaka yangu, tulikuwa tunaona miezi miandamo mitatu katika kipindi cha miezi miwili bila kuwasha moto (wa kupikia chakula) katika nyumba za mtume ﷺ", Naye akauliza: "Oo shangazi, mlikuwa mnakula nini ili muishi? Naye akasema: "tulikuwa tukiishi kwa kula vitu viwili vyeusi, navyo ni tende na maji, lakini Mtume ﷺ alikuwa na baadhi ya majirani wa kianswar[1] ambao walikuwa wana ngamia wa maziwa na walikuwa wakimletea Mtume ﷺ", maziwa ya ngamia hao.[2]".**
- **"Sahli ibni Saadi, mmojawapo wa wafuasi wa Muhammad ﷺ, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, hajauona mkate uliotengezwa kwa ngano nzuri sana tangu wakati alipotumwa na Mwenyezi Mungu (akiwa ni mtume) hadi anafariki."**

---

[1] *Ansar* ni wafuasi wa Mtume ambao ni wenyeji wa Madina, ambao walimpokea na kumnusuru Mtume.
[2] Saheeh Muslim, #2972, vilevile angalia, Saheeh Al-Bukhari, #2567.

- **Aisha, mke wa Muhammad, amesema: “Godoro la Mtume ﷺ, alilokuwa akilalia, lilikuwa limetengenezwa kwa ngozi na kujazwa kwa nyuzi nyuzi za madifu ya Mtende”.[1]**
- **Amr Ibn Al-Harith, ni mmoja wa wafuasi wa Muhammad ﷺ, amesema kuwa wakati Mtume ﷺ, alipofariki dunia, hakuacha fedha wala kitu kingine chochote ispokuwa nyumbu (baghla-mule)[2] wake mweupe aliekuwa akimpanda, silaha yake na kipande cha ardhi ambacho alikitoa sadaka.[3]”.**

Muhammad ﷺ aliishi maisha haya magumu mpaka ameaga dunia, ingawa hazina ya mali ya waisilamu ilikuwa chini ya usimamizi wake, sehemu kubwa ya bara Arabu ya uarabuni ilikuwa ni maeneo ya Uislamu kabla hajafariki, na waisilamu walikuwa ni washindi baada ya miaka kumi na minane ya kazi yake ya utume.

Je inawezekana kuwa Muhammad ﷺ alidai utume ili apate madaraka, utukufu, na nguvu? Tamaa ya kustarehe na madaraka na nguvu mara nyingi inafungamana na chakula kizuri, mavazi ya kifahari, makasri makubwa, walinzi wakakamavu, na mamlaka yasiopingwa. Je sifa yeyoto katika hizo inahusiana na Muhammad ﷺ? Muono mdogo unaofuata kuhusiana na maisha yake unaweza kusaidia kujibu swali hili.

Pamoja na majukumu yake akiwa, ni mtume, mwalimu, mkuu wa dola na ni hakimu, Muhammad ﷺ alikuwa akimkama mbuzi wake yeye mwenyewe, alikuwa akitia viraka nguo zake na

---

[1] Saheeh Muslimu, #2082, na Saheeh Al-Bukhari, #6456.
[2] Mnyama aliezaliwa kwa kuchanyanga kati ya farasi na punda.
[3] Saheeh Al-Bukhari, #2739, na Mosnad Ahmad, #17990.

kutengeneza viatu vyake, alikuwa akisaidia kazi za nyumbani, na kutembelea maskini walipokuwa wagonjwa. Vilevile aliwasaidia wafuasi zake kuchimba handaki kwa kusomba mchanga akiwa pamoja nao yeye mwenyewe. Maisha yake yalikuwa ni ya mtindo wa kustaajabisha wa hali ya chini na unyenyekevu.

Wafuasi wa Muhammad ﷺ walimpenda, walimuheshimu, na walimuamini kwa upeo wa kustaajabisha. Lakini bado alikuwa anaendelea kusisitizia kuwa ibada inatakiwa ielekezwe kwa Mwenyezi Mungu na wala sio kwake yeye binafsi. Anasi, mmoja wa maswahaba wa Muhammad ﷺ, amesema kuwa hakukuwa na mtu waliempenda sana kuliko Muhammad ﷺ, lakini, wakati Muhammad ﷺ alipowaendea, hawakumsimamia, kwa sababu Mtume alikuwa anachukia kuona wanamsimamia, kama wafanyavyo watu wengine kwa wakubwa zao[1].

Kipindi kirefu kabla ya kuwepo kwa mtazamo wa kufanikiwa kwa Uislamu na mwanzoni mwa muongo mrefu wa kuhuzunisha, mateso, maumivu, na kuudhiwa Muhammad ﷺ pamoja na wafuasi wake kwa ajili ya dini, Otba, alimuendea Muhammad ﷺ na kumwambia: "...Kama unataka mali, sisi tutakukusanyia mali ya kukutosha ili uwe tajiri kuliko sisi sote. Na kama unataka madaraka, tutakufanya uwe kiongozi na kamwe hatutotoa uamuzi wa jambo lolote bila ya idhini yako. Na kama unataka ufalme, tutakuvisha taji uwe mfalme wetu..." Na Muhammad ﷺ alitakiwa akubali jambo moja tu liwe ndio malipo ya ahadi hizo, nalo ni kutupilia mbali wito wa kuwalingania watu kuingia katika Uislamu na kumuabudu Mungu peke yake bila ya mshirika. Je ahadi hii haikuwa ni ya kushawishi kwa yeyote anaefuatilia manufaa ya kilimwengu? Je Muhammad ﷺ

[1] Mosnad Ahmad, #12117, pia katika Tirmizi,#2754.

alikuwa ni mwenye kusitasita ilipotolewa ahadi hii? Je aliishusha ahadi hiyo iwe kama ni aina ya mikakati ya kupatana bei huku akiuacha wazi mlango wa makubaliano ili apate ahadi nzuri zaidi ya hiyo? Lifuatalo ndilo lilokuwa jibu lake: **{ kwa jina la mwenyezi mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu }** Na akamsomea Otba aya za Qur'an, 41:1-38.[1] Na zifuatazo ni baadhi ya aya hizo:

> **﴾H'a Mim, Uteremsho huu umetoka kwa Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu, Hichi ni Kitabu kilicho pambanuliwa Aya zake, cha kusomwa kwa Kiarabu kwa watu wanao jua, Kitoacho khabari njema, na chenye kuonya. Lakini wengi katika wao wamepuuza; kwa hivyo hawasikii﴿ Qur'an, 41:1-4.**

Katika tukio lingine na akiwa katika kujibu ombi la baba yake mdogo la kumtaka aache kuwaita watu kuingia Uislamu, jibu la Muhammad ﷺ lilikuwa ni la kukata shauri na ni la dhati: **{Naapa kwa jina la Mungu, ee baba mdogo! kama wangeweka jua katika mkono wangu wa kulia na mwezi katika mkono wangu wa kushoto ili niache jambo hili la (kuwaita watu katika Uislamuu), kamwe sito acha mpaka ima Mungu aamuwe jambo hilo lishinde au niangamie kwa kulilinda jambo hilo}[2]."**

Muhammad ﷺ na wafuasi wake wachache, sio tu kuwa walisumbuka kutokana na mateso kwa muda wa miaka kumi na tatu, lakini pia makafiri walijaribu kutaka kumuua Muhammad ﷺ kwa mara kadhaa. Katika tukio mojawapo walijaribu kumuua kwa

---

[1] Kitabu: Al-Serah Al-Nabaweyyah, Ibn Hesham, Vol. 1, ukurasa wa, 293-294.
[2] Al-Serah Al-Nabaweyyah, Ibn Hesham, Vol. 1, ukurasa wa, 265-266.

kumdondoshea jiwe kubwa, ambalo lingemuangukia kichwani mwake[1], na mara nyingine walijaribu kumuua kwa kumtilia sumu katika chakula chake[2]. Nini kinachoweza kutetea uhalali wa maisha ya kusafa na kujitoa muhanga kama hayo hata baada ya ushindi dhidi ya wapinzani wake? Nini kinachoweza kufafanua maana ya unyenyekevu na wema ambao alioudhihirisha katika zama zake tukufu sana pale aliposistizia kuwa mafanikio yanatokana na msaada wa Mwenyezi Mungu tu na sio kutoka kwenye uhodari wake binafsi? Je hizi ndio tabia za mtu mwenye njaa ya madaraka au mbinafsi?

## (7) Ukuaji wa ajabu wa Uislamu

Mwishoni mwa sura hii, itakuwa ni jambo la kufaa sana tukionyesha dalili muhimu za ukweli wa Uislamu. Ni jambo mashuhuri sana ndani ya USA na dunia nzima kuwa, Uislamu ndio dini inayokua haraka mno kuliko dini zote. Ufuatao ni baadhi ya uchunguzi juu ya tikio hilo la ajabu:

- "Uislamuu ndio dini inayoenea kwa kasi zaidi Marekani, nayo ni muongozo na nguzo thabiti kwa watu wetu wengi..."(Hillary Rodham Clinton, *Los Angeles Times).*[3]
- "Waislamu ndio kundi linalokua kwa kasi kubwa duniani..." (The Population Reference Bureau, *USA Today*).[4]
- "....Uislamuu ndio dini inayokua kwa haraka sana katika nchi hii." (Geraldine Baum; muandishi wa habari za dini wa gazeti la Newsday).[5]

---

[1] Al-Serah Al-Nabaweyyah, Ibn Hesham, Vol. 1, ukurasa wa, 298-299
[2] Al-Daremey, #68, na pia angalia: Abu-Dawood, #4510.
[3] Larry B. Stammer, Muandishi wa mambo ya dini wa *Times, Los Angeles Times,* Home Edition, Metro Section, Part B, May 31, 1996, ukurasa wa, 3.
[4] Timothy Kenny, "Elsewhere in the World," *USA Today,* News Section, Toleo la Mwisho, February 17, 1989, ukurasa wa, 4A.
[5] Geraldine Baum, "For love of Allah," *Newsday,* Nassau and Suffolk Edition, News Section, Part II, March 7, 1989, ukurasa wa, 4.

▪ "Uislamuu, ni dini inayoenea kwa haraka zaidi Marekani..." (Ari L. Goldman, *New York Times).*[1]

Jambo hili la kustaajabisha, linaonyesha kuwa Uislamuu ni dini ya Mungu iliyo ya kweli. Haingii akilini kudhania kuwa Wamarekani wengi na watu wa kutoka nchi tofauti tofauti wamesilimu na kuingia katika Uislamu bila kufikiria kwa makini na kutafakari kwa kina kabla ya kuhitimisha kuwa Uislamu ni dini ya kweli. Huu ubadilishaji wa dini umetokea katika nchi mbali mbali, matabaka mbali mbali, makabila mbali mbali, na kazi za kimaisha mbali mbali. Wakiwemo wanasayansi, maprofesa, wanafalsafa, waandishi wa habari, wanasiasa, wasanii, na, wanariadha.

Pointi zilizotajwa katika sura hii zinajenga baadhi ya ushahidi tu unaounga mkono imani ya kuwa Qur'an ni maneno halisi ya Mungu, na kuwa Muhammad (S.AW) ni Mtume wa kweli alietumwa na Mungu, na kuwa dini ya Kiislamu ni dini ya kweli ya Mwenyezi Mungu.

❋❋❋

---

[1] Ari L. Goldman, Muandishi wa Gazeti la New York Times, Late City toleo la Mwisho, February 21, 1989, ukurasa wa, 1.

## Sura 2

# BAADHI YA FAIDA ZA UISLAMU

Uislamuu unatoa faida nyingi kwa mtu mmoja mmoja na kwa jamii nzima. Sura hii inataja baadhi ya faida zinazopatikana kupitia Uislamu kwa kila mmoja.

## (1) Mlango wa Kuingia Peponi

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

**﴾Na wabashirie walio amini na wakatenda mema kwamba watapata mabustani yapitayo mito kati yake......﴿ Qur'an, 2:25**

Vilevile Mwenyezi Mungu ameasema:

**﴾Kimbilieni msamaha wa Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyo wekewa walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake....﴿ Qur'an, 57:21**

Mtume Muhammad ﷺ ametueleza ya kwamba mtu wa daraja la chini kabisa miongoni mwa watu wa Peponi atakuwa na pepo ya ukubwa wa mara kumi ya ukubwa wa dunia,[1] na atapata kila kitu

[1] Saheeh Muslim, #186, na Saheeh Al-Bukhari, #6571.

anachotamani kikiwa ni zaidi ya mara kumi ya alichokitamani.[1] Vilevile Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{ Sehemu ndogo ya Pepo yenye ukubwa sawa na futi moja ni bora kuliko dunia[2] na vilivyomo ndani yake[3]} Vilevile amesema: {Peponi kuna vitu ambavyo hakuna jicho lililowahi kuviona, hakuna sikio lilowahi kuvisikia na hakuna mtu yeyote aliewahi kuvifikiria[4]} Vilevile amesema: {Mtu mwenye hali ngumu sana duniani miongoni mwa watu wa Peponi ataingizwa Peponi. Kisha ataulizwa: "Ewe mwanadamu, je umeshawahi kuona maisha ya shida? je umeshawahi kupata ya maisha ya dhiki?" Naye atasema: "Hapana, Naapa kwa Mwenyezi Mungu, Ee Mola! Kamwe sijawahi kukabiliana na maisha ya shida, na kamwe sijawahi kupata maisha ya dhiki."}**

Kama utaingia Peponi, utaishi maisha ya furaha sana bila kuumwa, kupata maumivu, huzuni, wala kufa; Mwenyezi Mungu atakuridhia nawe utaishi humo milele. Mwenyezi Mungu amesema katika Qu'an:

> **﴾Na wale walio amini na wakatenda mema tutawaingiza katika Pepo zipitazo mito kati yake kwa kudumu humo milele. Huko watakuwa na wake walio takasika, na tutawaingiza katika vivuli vizuri kweli﴿ Qur'an, 4:57**

[1] Saheeh Muslim, #188, na Mosnad Ahmad, #10832.
[2] Saheeh Al-Bukhari, #6568, na Mosnad Ahmad, #13368.
[3] Akimaanisha kuwa kama mtu atapewa sehemu ndogo sana katika pepo sawa na unyayo wa mtu basi mtu huyo atafaidika zaidi kuliko kama angepewa dunia nzima na vilivyomo ndani yake hii ni kuonyesha thamani ya ubora wa pepo, neema zake, na raha zake
[4] Saheeh Muslim, #2825, na Mosnad Ahmad, #8609.

(Tafadhali tembelea www.islam-guide.com/hereafter kwa maelezo zaidi kuhusu Pepo au Maisha baada ya kifo.)

## (2) Wokovu wa Kuepukana na Moto

Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **❮Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeli itoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru❯ Qur'an, 3:91**

Kwahiyo, maisha haya ni nafasi yetu ya pekee ya kushinda ili tuingie Peponi na tuepukane na Moto, kwasababu kama mtu atafariki ili hali ni Kafiri (haamini Uislamu), hatopata nafasi ya kurudi duniani kwa mara nyengine tena ili aje aamini. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu alivyoeleza katika Qur'an kuhusiana na kitu kitakachowatokea watu wasioamini katika siku ya kiyama:

> **❮Na unge ona watakapo simamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungeli rudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa miongoni wa Waumini❯. Qur'an, 6:27**

Lakini hakuna mtu yeyote atakaekuwa na nafasi hiyo ya pili.

Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{Mtu mwenye furaha sana duniani miongoni mwa watu watakaoingia Motoni katika Siku ya Kiyama, ataingizwa Motoni mara moja kisha ataulizwa: "Ewe binadamu je umeshawahi kuona kitu kizuri?**

**Je umeshawahi kupata kuwa na heri?" Naye atasema: "Hapana, Naapa kwa Mwenyezi Mungu, Oo Mola!"}**[1]

# (3) Furaha ya Kweli na Amani Moyoni

Furaha ya kweli na amani inaweza kupatikana katika kutii amri za Muumba na Mmiliki wa ulimwengu Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:



> **《Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwakumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyohutua!》 Qur'an, 13:28**

Kwa upande mwengine, yule atakaeiacha Qur'an atakuwa na maisha ya tabu hapa duniani. Mwenyezi Mungu amesema:

> **《Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu》. Qur'an, 20:124**[2]

Jambo hili linaweza kufafanua ni sababu gani zinazowafanya baadhi ya watu wajiue wakati wanafurahia (wanatesa) kuwa wana vitu vya kuwaliwaza na pesa za matumizi. Kwa mfano, mtazame Cat Stevens (kwa sasa ni Yusuf Islam), zamani alikuwa ni mwanamuziki mashuhuri wa muziki wa *Pop* ambaye alikuwa wakati mwingine akiingiza zaidi ya dola za kimarekani 150,000 kwa usiku mmoja. Baada ya kubadili dini na kuwa Muislamu, alipata furaha na amani

---

[1] Saheeh Muslim, #2807, na Mosnad Ahamad, #12699.

[2] Hawajaamini wala hawatendi kulingana na maagizo ya Qur'an.

ya kweli, ambayo alikuwa hajawahi kuipata katika mafanikio yake ya kiuchumi.[1]

Kwa kujisomea habari za watu waliosilimu na kuingia Uislamu, tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/stories au rejea kitabu kiitwacho: *Why Islam is Our Only Choice*[2]*,(kwa nini Uislamu ndio chaguo letu la pekee).* Katika ukarasa huu wa mtandao na katika kitabu hiki, unaweza kujisomea fikira na mawazo ya watu hao, ambao ni watu wa nchi mbalimbali na wana historia na viwango vya elimu tofauti tofauti.

## (4) Msamaha wa Dhambi Zote Zilizotangulia

Pindi mtu anaposilimu, Mwenyezi Mungu anamsamehe dhambi na matendo yake maovu yote yaliyotangulia. **Mtu aitwae Amr alienda kwa Mtume Muhammad ﷺ na akamwambia: "Ninyooshee mkono wako wa kulia ili nile kiapo cha kukuunga mkono." Mtume ﷺ akanyoosha mkono wake wa kulia. Amr akaondoa mkono wake. Mtume ﷺ akasema: { Oo Amr Una nini?} Nae akajibu: "Nilinuia kuweka sharti." Mtume ﷺ akamuuliza {Ni sharti gani ulilokusudia kuliwasilisha?} Amr akasema: "Nalo ni kwamba Mwenyezi Mungu anisamehewe dhambi zangu." Mtume ﷺ akasema: {Hivi ulikuwa hujui kuwa kuingia Uislamu kunafuta madhambi yote yaliyotangulia[3]?}**

---

[1] The present mailing address of Cat Stevens (Yusuf Islam), kama ukitaka kumuuliza kuhusu hisia zake baada ya kuingia Uislamu nayo ni: Digswell Street, London N7 8JX, United Kingdom.
[2] Kitabu hiki kimetungwa na Muhammad H. Shahid. Kwa kujipatia Nakala ya kitabu hiki tafadhali tembelea www.islam-guide.com/stories
[3] Saheeh Muslim, #121, vilevile katika Mosnad Ahmad, #17357.

Baada ya kuingia Uislamu, mtu atalipwa matendo yake mazuri au mabaya kulingana na kauli ya Mtume Muhammad ﷺ ifuatayo: **{Mola wako, ambaye ni Mwenye kubariki na ni Mwenye kutukuza, ni Mwenye rehema sana. Kama mtu anakusudia kutenda jema lakini hajalitenda, basi ataandikiwa tendo jema. Na kama akilitenda, (malipo yake) ni kuanzia mara kumi hadi mara mia saba au zaidi (ikiwa ni malipo ya tendo jema moja), ataandikiwa mtu huyo. Na kama mtu anakusudia kutenda ovu lakini hajalitenda, ataandikiwa tendo jema. Na kama atalifanya, ataandikiwa dhambi moja au Mwenyezi Mungu anaweza kumfutia.}**[1]

✵✵✵

[1] Mosnad Ahmad, #2515, na Saheeh Muslim, #131,

Sura 3

# MAELEZO YA JUMLA JUU YA UISLAMU

## Uislamu Ni Nini?

Dini ya Kiisilamu ni kukubali na kutii mafundisho ya Mungu aliyoyashusha kwa Mtume wake wa mwisho, Muhammad ﷺ.

## Baadhi ya Misingi ya Imani ya Kiisilamu

### 1) Kumuamini Mwenyezi Mungu:

Waislamu wanaamini Mungu ni mmoja, mpweke, Mungu asiefanana na chochote ambae hana mwana wala mke, na kuwa hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila yeye. Yeye peke yake ndiye Mungu wa kweli, na miungu mingine yote ni ya uwongo. Yeye ana Majina matukufu na Sifa tukufu za ukamilifu. Hakuna mtu anaeshirikiana naye kiuungu, wala sifa zake hizo. Mwenyezi Mungu amejieleza, Katika Qur'an:

**﴾Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja.﴿ Qur'an, 112:1-4**



*Sura ya 112 ya Qur'an, iliyoandikwa kwa hati ya kiufundi ya kiarabu.*

Hakuna mtu mwenye haki ya kuombwa dua, kunyenyekewa, kuelekezewa sala, au kuonyeshwa tendo lolote la kuabudiwa, kinyume na Mwenyezi Mungu Peke yake.

Mwenyezi Mungu Pekee ndiye Mwenye nguvu, Muumba, Mfalme, na ndiye mpaji wa kila kitu ulimwenguni. Yeye ndie muendeshaji wa mambo yote. Hategemei chochote katika viumbe vyake, na viumbe vyake vyote vinamtegemea kwa yote wanayoyahitaji. Yeye ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona na ni Mjuzi wa kila kitu. Ikiwa katika hali ya ukamilifu, elimu yake imekizunguka kila kitu, kilicho wazi na kilichofichikana, kitu cha umma au cha binafsi. Anajua yaliyotokea, yatakayo tokea na namna gani yatakavyotokea. Hakuna jambo linalotokea katika ulimwengu wote ispokuwa linatokea kwa matakwa yake. Chochote atakacho ndicho huwa, na chochote asichokitaka hakiwi na kamwe hakitakuwa. Matakwa yake yapo juu ya matakwa ya viumbe vyake. Yeye ana nguvu juu ya kila kitu, na anaweza kufanya kila kitu. Yeye ni Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu na ni Mwenye kuneemesha. Katika moja ya hadithi za Mtume Muhammad ﷺ tumeambiwa kuwa Mungu ni Mpole (Rahimu) sana kwa viumbe vyake kuliko upole wa mama kwa mwanawe.[1] Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuepukana na dhulma na uonevu. Yeye ni Mwenye Hekima katika matendo na maamrisho yake yote. Kama mtu anataka kitu kutoka kwa Mungu, anaweza kumuomba Mungu moja kwa moja bila ya kumtaka mtu mwingine yeyote amuombee kwa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu sio Yesu, na Yesu sio Mungu[2]. Hata Yesu Mwenyewe ameyakana hayo ya kuwa yeye ni Mungu. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

---

[1] Saheeh Muslim, #2754 na Saheeh Al-Bukhari, # 5999.

[2] Mnamo tarehe 25 june 1984, Wakala wa gazeti la Press London, ulitangaza kuwa asilimia kubwa ya Maaskofu madhehebu ya kanisa la Anglikana walipokuwa katika vipindi vya dini walisema:" hakuna haja kwa Wakristo kuamini kuwa Yesu

**﴾Hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni Masihi mwana wa Maryamu! Na hali Masihi mwenyewe alisema: Enyi Wana wa Israili! Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru.........﴿ Qur'an, 5:72-75**

Mungu si Utatu Mtakatifu. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

**﴾Kwa hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna mungu ila Mungu Mmoja. Na ikiwa hawaachi hayo wanayo yasema, kwa yakini itawakamata adhabu chungu wale wanao kufuru......﴿ Qur'an, 5:73-75**

Uislamu unapinga madai kuwa Mungu alipumzika katika siku ya Saba ya kuumba, na eti Mungu alipigana mieleka na mmoja wa Malaika zake, na kuwa Mungu ni Mpangaji njama Mwenye chuki dhidi ya binadamu, au kuwa ana Umbo la binadamu. Vile vile Uislamuu unapinga sifa za mtu yeyote zenye mfano na Mungu. Madai yote hayo yanazingatiwa kuwa, ni kumkufuru Mwenyezi Mungu. Mungu ni Mtukufu. Yeye ameepukana kabisa na upungufu. Yeye kamwe hatochoka. Yeye Hasinzii wala halali.

---

alikuwa ni Mungu," Idadi ya Maaskofu hao wa Kianglikana ilikuwa ni 31 kati ya idadi ya Maaskofu wote 39 wa England (Uingereza) Msemaji mkuu wa Maaskofu hao 31 wa Kianglikana alisema kuwa Maaskofu 19 kati ya 31 wa Kianglikana, wamesema kuwa inatosha kuamini kuwa "Yesu alikuwa ni Wakili Mkuu wa Mungu"

Neno la kiarabu ***Allah*** lina maana ya Mungu (mmoja na ni Mungu wa kweli pekee aliyeumba Ulimwengu wote). Neno hili ***Allah*** ni jina la Mwenyezi Mungu, ambalo linatumika na wazungumzaji wote wa kiarabu, wawe waislamu au wakristo. Neno hili haliwezi kutumika kuashiria kitu chchote zaidi ya Mungu wa kweli aliye mmoja. Na neno la kiarabu ***Allah*** limetajwa katika Qur'an zaidi ya mara 2150. Katika lugha ya Aramaic, lugha ambayo inafungamana kwa karibu sana na lugha ya kiarabu na ndio lugha ambayo aliitumia Yesu katika mazungumzo yake[1], katika lugha hiyo Mungu anaitwa Allah vile vile.

## 2) Kuamini Malaika:

Waislamu wanaamini kuwepo kwa Malaika na kuwa Malaika hao ni Viumbe wema. Malaika wanamuabudu Mungu peke yake, wanamtii, na wanatenda kwa mujibu wa amri zake tu. Miongoni mwa Malaika kuna Malaika Jibrili (Gabriel) ambaye ndie aliyeshusha Qur'an kwa Muhammad ﷺ.

## 3) Kuamini Vitabu Vilivyofunuliwa na Mungu:

Waislamu wanaamini kuwa Mwenyezi Mungu ameshusha Vitabu kwa Mitume yake vikiwa ni kama Uthibitisho kwa watu na ni muongozo wao. Miongoni mwa Vitabu hivyo ni Qur'an, ambayo, Mwenyezi Mungu ameiteremsha kwa Mtume Muhammad ﷺ. Mwenyezi Mungu amechukua dhamana ya kuilinda Qur'an kutokana na uharibifu au mabadiliko ya aina yoyote. Mwenyezi Mungu amesema:

---

[1] *New International Version*, *NIV Compact Dictionary of the Bible, Douglas*, ukurasa wa, 42.

**❮Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda❯ Qur'an, 15:9**

## 4) Kuamini Mitume na Manabii wa Mungu:

Waislamu wanaamini Mitume na Manabii wote wa Mungu, kuanzia Adam, na akiwemo Nuhu, Ibrahimu, Ismaili, Isaaka, Yakubu, Musa na Yesu (Rehema na amani ziwe juu yao). Lakini ujumbe wa mwisho ulioletwa kwa watu, ambao ndio unaoimarisha ujumbe wa milele, ulifunuliwa kwa Mtume Muhammad ﷺ. Waisilamu wanaamini kuwa Muhammad ndiye Mtume wa mwisho aliyetumwa na Mungu, kama Mungu alivyosema:

**❮Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu❯. Qur'an, 33:40**

Waislamu wanaamini kuwa Manabii na Mitume wote waliumbwa wakiwa ni wanadamu ambao hakuna hata mmoja kati yao mwenye sifa za Uungu.

## 5) Kuamini Siku ya Mwisho (Siku ya hukumu):

Waislamu wanaamini kuwa ipo siku ya Mwisho (Siku ya kiyama), Siku ambayo watu wote watafufuliwa kwa ajili ya hukumu ya Mungu kulingana na Imani na matendo yao.

## 6) Kuamini Kadari ya Mungu (majaaliwa ya Mwenyezi Mungu):

Waislamu wanaamini kuwepo kwa Kadari,[1] ambayo ni majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, Lakini imani hii ya kuamini majaaliwa ya Mwenyezi Mungu haina maana kuwa binadamu hawana hiari. Bali waislamu wanaamini kuwa Mwenyezi Mungu amempa binadamu uhuru wa kufanya anachotaka. Hii ikiwa na maana ya kuwa binadamu ana uwezo wa kuchagua jema au baya, na kuwa binadamu wataulizwa kutokana na machaguo yao.

Imani ya kuamini majaaliwa ya Mwenyezi Mungu inakusanya imani ya vitu vinne: 1) Mwenyezi Mungu anajua kila kitu. Anajua kilichotokea na kitakachotokea. 2) Mwenyezi amesharekodi mambo yote yaliyotokea na yatakayotokea. 3) Chochote anachokitaka Mungu kiwe ndicho kitakachokuwa na chochote asichokitaka kiwe kamwe hakitokuwa. 4) Mwenyezi Mungu ni Muumba wa kila kitu.

(Tafadhali tembelea www.islam-guide.com/beliefs kwa maelezo zaidi kuhusu misingi ya imani ya Kiislamu)

## Je kuna Chanzo Kitakatifu KingineZaidi ya Qur'an?

Ndio, nacho ni Sunna (yaani yale yaliosemwa na Mtume Muhammad ﷺ, aliyoyatenda, au kuyathibitisha) ni chanzo cha pili cha sheria za Kiislamu. Sunna zimekusanya *hadithi*, ambazo ni habari zilizonukuliwa kwa njia za kuaminika na wafuasi wa Mtume Muhammad ﷺ habari za kile alichosema, tenda au kukiafiki. Kuamini *sunna* ni msingi wa imani ya Kiisilamu.

[1] Kadari ya Mungu ni Uwezo wake juu yetu, kuwa kuna mambo mengi yanamtokea binadamu bila kupenda kwake kwa mfano: Kuumwa au kupata ajali, Utajiri na Umasikini, Uhai na Mauti, yote ni Mipango ya Mungu (Kadari)

# Mifano ya Maneno ya Mtume Muhammad ﷺ

- **{Mfano wa waumini, jinsi wanavyopendana, kuhurumiana na kufanyiana wema baina yao ni sawa na mfano wa Mwili wa binadamu: kama kiungo kimoja cha Mwili huo kitauma basi mwili wote utakesha kwa homa[1]}**
- **{Waumini wakamilifu zaidi kiimani ni wale walio na tabia nzuri zaidi, na Waumini walio bora zaidi miongoni mwao ni wale wanaowatendea vyema wake zao[2]}**
- **{Hawi mmoja wenu na imani kamilifu mpaka pale atakapompendelea ndugu yake kile anachokipenda yeye[3]}**
- **{Wenye huruma uhurumiwa na Mungu mwenye wingi wa huruma. Wahurumieni walio ardhini mtahurumiwa na alie mbinguni[4] (yaani Mungu)}**
- **{Kumtabasamia ndugu yako ni sadaka...[5]}**
- **{Neno zuri ni sadaka[6]}**
- **{Mwenye kumuamini Mungu na Siku ya Kiyama basi amtendee wema Jirani yake[7]}**
- **{Mwenyezi Mungu haangalii Miili yenu wala Sura zenu lakini anaangalia Mioyo yenu na Matendo yenu[1]}**

---

[1] Saheeh Muslim,#2586, pia katika: Saheeh Al-Bukhari, #6011.
[2] Mosnad Ahmad, #7354, pia katika: Al-Tirmizi, #1162.
[3] Saheeh Al-Bukhari, #13 na katika Saheeh Muslim, #45
[4] Al-Tirmizi, #1924 na katika: Abu-Dawood, #4941.
[5] Al-Tirmizi, #1956.
[6] Saheeh Muslim, #1009, na katika: Saheeh Al-Bukhari, #2989.
[7] Saheeh Muslim, #48 na katika: Saheeh Al-Bukhari, #6019.

- **{Mlipe Mfanyakazi ujira wake kabla jasho lake halija kauka}[2]**
- **{Kulikuwa na mtu anatembea njiani akashikwa na kiu kali sana. Akakipata kisima, akaingia katika kisima hicho na akanywa kiasi cha kumtosha kisha akatoka. Ghafla akamuona mbwa anahaha huku katoa ulimi nje kwa kiu kali iliyompata mpaka anakula matope, yule mtu akasema: "Mbwa huyu ameshikwa na kiu kali kama ile iliyonishika mimi. "Hivyo basi akaingia tena kisimani akajaza maji katika kiatu chake kisha akamnywesha yule mbwa, Mwenyezi Mungu akampa yule mtu ahsante yake (malipo mema) na akamsamehe dhambi zake. Mtume aliulizwa: "Ewe Mtume wa Mungu, hivi sisi tunapata malipo kwa kuwafanyia wema wanyama? Mtume ﷺ akajibu: "Kuna malipo kwa kila jema mnalowatendea wanyama hai au binadamu}[3].**

## Uislamu unasema nini kuhusu siku ya Kiyama?

Kama walivyo Wakristo, Waislamu wanaamini kuwa haya maisha ya duniani ni maandilizi na majaribio tu kwa maisha ya baadae. Maisha haya ya kidunia ni mtihani kwa kila mtu kwa ajili ya maisha ya baada ya kifo. Siku ikifika ulimwengu wote utaangamizwa na wafu watafufuliwa ili wakahukumiwe mbele ya Mungu. Siku hiyo itakuwa ndio mwanzo wa maisha yasiyo na mwisho. Siku hiyo ni Siku ya Hukumu. Katika siku hiyo watu wote watalipwa na Mungu kulingana na itikadi zao na matendo yao. Wale waliokufa wakiwa na

---

[1] Saheeh Muslim, #2564.
[2] Ibn Majah, #2443.
[3] Saheeh Muslim, #2244. na katika: Saheeh Al-Bukhari, #2466.

imani ya kuwa “Hakuna Mola wa kweli ila Mwenyezi Mungu, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Mungu.” na ni Waisilamu, watalipwa katika siku hiyo na wataingizwa Peponi na kuishi humo milele, Kama Mwenyezi Mungu alivyosema:

**﴾Na wale walio amini na wakatenda mema, hao ndio watu wa Peponi, humo watadumu﴿ Qur’an, 2:82**

Ama wale ambao walifariki dunia wakiwa hawaamini kuwa “Hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na kuwa Muhammad ni Mtume wa Mungu” au hawakuwa Waisliamu, wataikosa Pepo milele na wataingizwa Motoni (kuzimu). Kama Mwnyezi Mungu alivyosema:

**﴾Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamuu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri﴿ Qur’an,3:85**

Na kama alivyosema:

**﴾Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeli itoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru﴿ Qur’an, 3:91**

Mtu anaweza kuuliza,"Naona Uislamu ni dini nzuri, Lakini kama nitasilimu, familia yangu, marafiki zangu na jamaa wengine watanisumbua na watanibeza. Je kama sitosilimu nitaingia Peponi na kuepuka Motoni?

Jibu ni kile alichokisema Mungu katika aya iliyotangulia: **❰Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamuu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri kupata hasara❱ Qur'an,3:85**

Baada ya kumleta Mtume Muhammad ﷺ kuja kuwalingania (kuwaita) watu kuingia Uislamu, Mwenyezi Mungu hakubali ufuasi wa dini yeyote kinyume na Uislamu. Mwenyezi Mungu ni Muumba wetu na Mpaji wetu. Ametuumbia kila kitu duniani. Baraka zote na vitu vizuri vyote tupatavyo vinatoka kwake. Halafu baada ya mambo yote hayo, mtu anakataa kumuamini Mwenyezi Mungu, na Mtume Muhammad ﷺ, au Dini yake ya Uislamu, ni haki kwa mtu huyo kuadhibiwa katika siku ya Kiyama. Kwa kweli, lengo kuu la kuumbwa kwetu ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Pekee na kumtii, kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika Qur'an tukufu, (51:56)

> **❰Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi❱ Qur'an, 51:56**

Maisha tunayoishi sasa ni mafupi mno. Makafiri, wakiwa katika Siku ya Kiyama watadhani kuwa maisha waliyoishi duniani yalikuwa ni siku moja tu au sehemu ya siku. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu:

> **❰Atasema: Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hisabu ya miaka? Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanao weka hisabu.❱ Qur'an, 23:112-113**

Na Mwenyezi Mungu amesema**:**

> **❰Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi**

**Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.﴿ Qur'an, 23:115-116**

Maisha ya Ahera ni maisha ya kweli. Nayo sio maisha ya kiroho tu lakini ni maisha ya kimwili pia. Tutaishi huko tukiwa na roho zetu na miili yetu. Akilinganisha dunia na Akhera, Muhammad ﷺ amesema: **{Thamani ya maisha ya dunia ukilinganisha na maisha ya Akhera ni sawa na maji utayoyapata ukiingiza kidole katika bahari kuteka maji.}**[1] Hiyo ndio thamani ya maisha ya dunia ukilinganisha na maisha ya Akhera nayo ni sawa na matone ya maji kidogo ukiyalinganisha na bahari.

## Vipi Mtu atakuwa Muislamu?

Ni rahisi aseme kwa uhakika, "*La ilaha illa Allah, Muhammadur rasoolu Allah*", Hapo atakuwa amesilimu na amekuwa Muislamu. Maneno haya yanamaanisha kuwa: "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mungu (Allah) na Muhammad ni Mtume wa Mungu. "Kifungu cha kwanza, "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mungu" kinamaanisha kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa kinyume na Mungu pekee, na kuwa Mungu hana mshirika wala Mwana. Ili kuwa Muislamu vile vile unatakiwa:

- Kuamini kuwa Qur'an tukufu ni maneno halisi ya Mwenyezi Mungu, yaliyoshushwa na Mungu.
- Kuamini kuwa Siku ya Kiyama (Siku ya kufufuliwa) ni kweli kuwa ipo na itafika, kama alivyoahidi Mwenyezi Mungu katika Qur'an.
- Kukiri kuwa Uislamu ndio dini yake.
- Usiabudu chochote wala yeyote ispokuwa Mwenyezi Mungu.

---

[1] Seheeh Muslim, #2858, na Mosnad Ahmad, #17560.

**Mtume Muhammad ﷺ amesema: {Mwenyezi Mungu huwa na furaha sana pale Mja wake anapotubu kwake kuliko furaha ya mmoja wenu kama angekuwa akimuendesha ngamia wake katika Msitu kisha ghafla Ngamia huyo akamtoroka, huku ngamia huyo akiwa na Maji na Chakula cha mtu huyo, kwa hiyo akakata tamaa ya kumpata tena. Huyo mtu akaenda katika Mti na akajilaza chini ya kivuli cha mti huo (akisubiri kifo), kwa kule kupoteza matumaini yote ya kumpata tena ngamia wake. Akiwa katika hali hiyo (ngumu) ghafla akamuona yule ngamia amesimama mbele yake! Kwa hiyo akashika hatamu zake na akalia kwa furaha, kisha akasema: {Ewe Mola Wewe ni Mja wangu na Mimi ni Mola wako" makosa ya matamshi yake yametokana na Furaha yake iliyokuwa kubwa,}**[1]

*Maneno "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wa Mungu". yalioandikwa juu ya lango.*



# Qur'an Inahusika na nini?

Qur'an ni Maneno ya mwisho kuteremshwa na Mwenyezi Mungu, nayo ni msingi wa kutegemewa wa imani na matendo ya kila Muislamu. Qur'an inazungumzia kadhia zote zinazowahusu wanadamu: hekima, itakadi, kuabudu, mapatano ya kibiashara, sheria, n.k., lakini Maudhui



[1] Saheeh Muslim, #2747, na Saheeh Al-Bukhari, #6309.

yake kuu ni uhusiano kati ya Mungu na viumbe vyake. Wakati huohuo, inatoa muongozo na mafundisho kamili ya jamii yenye uadilifu, maadili ya kiungwana yanayofaa, na mfumo wa uchumi wenye usawa.

Zingatia kwamba Qur'an imefunuliwa kwa Muhammad ﷺ kwa lugha ya kiarabu tu. Kwa hiyo tafsiri yoyote ile, iwe ya kingereza au lugha yoyote ile, sio Qur'an wala si toleo la Qur'an, lakini hiyo ni tafsiri tu ya maana ya Qur'an. Qur'an asilia ni ya kiarabu, lugha iliyoteremshiwa.

## Mtume Muhammad ﷺ Ni nani?

Muhammad ﷺ kazaliwa Makka mwaka 570 AD. Tangu kufariki kwa baba yake ikiwa ni kabla ya kuzaliwa kwake na mama yake naye alifariki muda mfupi tu baadaye, akalelewa na baba yake mdogo ambaye ametokea katika kabila tukufu la Quraysh. Mtume alilelewa akiwa hajui kusoma wala kuandika na akaendelea hivyo hivyo mpaka kifo chake. Watu wake, kabla ya kupewa kazi yake ya utume, walikuwa wajinga hawajui sayansi istoshe wengi wao walikuwa hawajui kusoma wala kuandika. Alipokuwa mkubwa akawa anafahamika kuwa ni muaminifu, mwema, mtegemewa, mkarimu, na ni mwenye moyo safi. Alikuwa ni mtu wa kutegemewa sana kiasi ambacho wakamuita Mkweli, Muaminifu. Muhammad ﷺ alikuwa ni mtu wa dini sana na alikuwa anachukia mno mmomonyoko wa maadili na ibada za masanamu zinazofanywa na jamii yake.

Muhammad ﷺ alipofikia umri wa miaka arobaini, alipokea ufunuo wake wa kwanza kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia Malaika Jibrili. Ufunuo uliendelea kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu, na huo ufunuo kwa makubaliano (ijimai) ya umma wote wa kiisilamu unajulikana kwa jina la Qur'an.



*Msikiti wa Mtume Muhammad ﷺ uliopo Maddinah.*


Mara tu alipoanza kuikariri Qur'an na kuhubiri ukweli aliofunuliwa na Mungu, yeye na kikundi kidogo cha wafuasi wake waliudhiwa kwa mateso na makafiri. Maudhi yakawa makali sana kiasi ambacho mnamo mwaka 622 AD. Mungu akawapa idhini ya kuhama. Uhamiaji huo wa kutoka Maka kwenda mji wa Madina, kiasi cha maili 260 kuelekea kaskazini ndio unaounda alama ya kuanza kwa kalenda ya kiislamu.

Baada ya miaka kadhaa, Muhammad ﷺ na wafuasi wake waliweza kurudi Makka, ambapo waliwasamehe maadui zao. Kabla ya kufariki Mtume Muhammad ﷺ akiwa na umri wa miaka sitini na tatu, sehemu kubwa ya bara Arabu ilikuwa ni ya kiislamu, na ndani ya karne moja tangu afariki, Uislamu ulisambaa hadi kufikia Hispania kwa upande wa magharibi na mpaka kufikia mashariki ya mbali nchini China. Miongoni mwa sababu kuu zilizopelekea kusambaa haraka na kwa amani kwa Uislamu ilikuwa ni ukweli na uwazi wa itakadi yake. Uislamu unawalingania watu waje katika imani ya kuabudu Mungu mmoja tu, ambaye ni mmoja tu peke yake anayestahiki kuabudiwa.

Mtume Muhammad ﷺ alikuwa ni mfano uliokamilika wa wema, udilifu, huruma, upole, uaminifu, na ushujaa. Ingawa alikuwa ni binadamu, aliepushwa na tabia mbaya zote na alijizatiti kikakamavu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na thawabu zake za kesho Akhera. Zaidi ya hayo, katika matendo yake yote na shughuli zake zote, alikuwa ni mzingatiaji na ni mcha Mungu.

Tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/muhammad Kwa Maelezo zaidi kuhusu Mtume Muhammad (S.A.W.)

## Kusambaa kwa Uislamu Kumeleta Athari gani katika Maendeleo ya kisayansi?




Uislamu unamfunza mtu atumie nguvu ya akili yake na uchunguzi. Katika kipindi cha miaka michache tu ya kusambaa kwa Uislamu, ustaarabu mkubwa na vyuo vikuu vilistawi. Muungano wa fikra za kimashariki na kimagharibi, na fikra mpya pamoja na za zamani zileleta maendeleo makubwa katika tiba, hisabati, fizikia, unajimu, Jiografia, ujenzi, sanaa, fasihi, na historia. Mifumo mingi ya maana sana, kama vile algebra, namba za kiarabu, na dhana ya matumizi ya sifuri (uhai wa wa maendeleo ya hisabati), ulipelekwa Ulaya ya zama za kati kutoka katika ulimwengu wa kiisilamu.Vyombo vya kisasa ambavyo vilirahisisha uwezekano wa misafara ya ugunduzi ya watu wa Ulaya,



***Astrolabe:*** *ni moja kati ya vyombo vya kisayansi vya muhimu sana kilichoendelezwa na Waislamu na ni chombo ambacho kilitumiwa sana katika nchi za Magharibi mpaka zama za kisasa.*

kama vile chombo cha (astrolabe) kitumikacho kupimia anga n.k., kipima pembe, na ramani nzuri za matumizi ya baharini, vile vile ziliendelezwa na waisilamu.



*Wanafizikia wa Kiislamu walitoa kipaumbele kwa mambo ya upasuaji na wakaviendeleza vifaa vingi vya upasuaji kama inavyoonekana katika mchoro huu wa kale.*

## Waislamu Wanaamini nini juu ya Yesu?

Waislamu wanamheshimu na kumstahi sana Yesu (Rehema na amani ziwe juu yake). Wanamzingatia kuwa ni mmoja wa Mitume mikuu ya Mungu aliyetumwa kuwaongoza watu. Qur'an inathibitisha uzawa wake wa kibikira, na kuna sura ya Qur'an iitwayo '*Maryam*' (Maria). Qur'an imeelezea uzazi wa Yesu kama ifuatavyo:

**﴾Na pale Malaika walipo sema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa walio karibishwa (kwa Mwenyezi Mungu.) Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema. Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huumba apendacho. Anapo hukumu jambo, huliambia: Kuwa! Likawa.﴿ Qur'an, 3:45-47**

Yesu alizaliwa kimiujiza kwa amri ya Mungu ambaye amemuumba Adam bila baba, Mwenyezi Mungu amesema:

**﴾Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; alimuumba kwa udongo kisha akamwambia: Kuwa! Basi akawa﴿ Qur'an, 3:59**

Katika kipindi cha kazi yake ya utume, Yesu alifanya miujiza mingi. Mungu anatueleza kuwa Yesu alisema:

**﴾...Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na**

**ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakwambieni mnacho kila na mnacho weka akiba katika nyumba zenu...》 Qur'an, 3:49**

Waislamu wanaamini kuwa Yesu hakusulubiwa. Ispokuwa ilikuwa ni njama za maadui zake ya kutaka kumsulubu, lakini Mwenyezi Mungu alimuokoa na kumpaisha akampeleka kwakwe juu. Na umbo linalofana na Yesu liliwekwa kwa mtu mwingine. Maadui wa Yesu wakamchukua mtu huyo na wakamsulubu wakidhani kuwa huyo ndiye Yesu. Mwenyezi Mungu amesema:

**《Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsalibu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuuwa kwa yakini.》 Qur'an, 4:157**

Si Muhammad ﷺ wala Yesu aliyekuja ili kubadilisha misingi ya imani ya kuamini Mungu mmoja, iliyoletwa na mitume iliyotangulia, lakini kinyume chake wamekuja kuithibitisha na kuitengeneza imani hiyo.[1]

---

[1] Waislamu wanaamini kuwa Mwenyezi Mungu aliteremsha Injili kwa Nabii Isa (Yesu) ambayo mpaka sasa inapatikana katika baadhi ya kitabu cha Biblia agano jipya, lakini hii haina maana kuwa Waislamu wanaamini Injili hii ya agano jipya , kwasababu haipo kama Mwenyezi Mungu alivyoishusha kwa Nabii Isa, hii inatokana na Mabadiliko kadhaa yaliyofanywa juu ya kitabu hicho ya kuondolewa baadhi ya Sura na kuchomekwa Sura nyengine. Kulingana na taarifa iliyotolewa na



*Msikiti wa Aqsa Jerusalem.*

(Tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/jesus Kwa Maelezo zaidi kuhusu Yesu katika Uislamu.

---

tume ya kitabu kitukufu cha Biblia, tume ambayo iliundwa na Wasomi 32 ambao ni wanaumoja wenye kuitumikia tume hiyo, wakiwa chini ya wajumbe 50 wenye kuhusika na maswala ya dini hiyo, baada ya kufanya Uchunguzi tume ya Wasomi hao ilisema kuwa katika *UTANGULIZI* wa kitabu kitukufu cha Biblia (*Holy Bible-standard Version*) ukurasa, iv kuna aya zimeondolewa: "hakika Nakala za Injili zimebadilishwa sana na hakuna hata Nakala moja iliyokuwa Salama, hivyo basi ni bora tutumie Nakala itakayotolewa na tume hii ya uchunguzi kwani itakuwa ndio Nakala iliyo karibu sana na Usalama na yenye kukaribiana sana na Nakala ya Asili" vilevile wakaweka alama za footnote kuonyesha Mabadiliko hayo yaliyofanywa katika (Mt 9.34; Mk 3.16; 7.4; Lk 24.32,51, etc). Kwa maelezo zaidi www.islam-guide.com/bible

# Uislamu Unasemaje kuhusu Ugaidi?

Uislamu, ni dini ya huruma, hairuhusu ugaidi. Mwenyezi Mungu amesema katika Qur'an:

> **﴾Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu.﴿ Qur'an, 60:8**

Mtume Muhammad ﷺ aliwakataza wanajeshi wasiwauwe wanawake na watoto,[1] na aliwahusia: **{msifanye usaliti, msiue kwa fujo, msiue watoto wachanga.} Vile vile amesema: {Yeyote atakayeua mtu mwenye mkataba wa amani na waisilamu hato nusa harufu ya Pepo, ingawa harufu ya Pepo inapatikani umbali wa miaka arobaini.}**[2]

Vilevile Mtume Muhammad amekataza adhabu ya kutumia moto.[3]

Mtume ﷺ ameorodhesha kuuwa kuwa ni dhambi kubwa ya pili,[4] na ameonya kuwa katika siku ya Kiyama, {**Kesi za mwanzo kuhukumiwa baina ya wanadamu zitakuwa kesi za umwagaji damu.}**

Waisilamu wanahimizwa wawatendee wema wanyama, na ni haramu kuwatesa. Wakati moja Mtume Muhammad ﷺ amesema:

---

[1] Kitabu: *Saheeh Muslim*, #1744, pia katika *Saheeh Al-Bukhari*, #3015.
[2] Saheeh Muslim, #3166, pia angalia Ibn Majah, #2686.
[3] Abu-Dawood, #2675. na Saheeh Muslim, #88.
[4] Saheeh Al-Bukhari, #6871,

**{Mwanamke mmoja aliadhibiwa kwa sababu alimfungia ndani paka mpaka akafa. Katika tukio hilo, mwanamke huyo aliingizwa motoni. Kwa vile alimfungia paka huyo, bila ya kumpa chakula wala maji, wala hakumuacha huru ajiliie wadudu.}**[1]

Vilevile amesema kuwa mtu mmoja alimpa maji mbwa mwenye kiu kali, kwa hiyo Mungu alimsamehe dhambi zake kwa tendo hilo. Mtume ﷺ aliulizwa: "Ewe Mtume wa Mungu, hivi sisi tunapata malipo kwa kuwafanyia wema wanyama?" Mtume akasema: **{Kuna malipo ya kila jema mnalowatendea wanyama hai au binadamu.}**

Kwa kuongezea, wakati wa kumchinja mnyama ili aliwe, Waisilamu wameamrishwa wamchinje kwa njia itakayompunguzia hofu na maumivu mnyama huyo. Mtume Muhammad ﷺ amesema: {Utakapo mchinja myama, basi fanya hivyo kwa njia nzuri. Mtu anatakiwa anoe kisu chake ili ampunguzie mateso huyo mnyama.}[2]

Kwa kuweka wazi maelezo hayo na maandiko mengine ya kiisilamu, tendo la kutia hofu katika mioyo ya raia wasio na ulinzi wowote ule, uharibifu mkamilifu wa majengo na vitu, kulipua mabomu, na kuwatia vilema wanaume, wanawake, na watoto wasio na hatia mambo yote hayo yamekatazwa na ni matendo yanayochukiwa sana na Uislamu na Waisilamu. Waisilamu wanafuata dini ya amani, huruma, na kusameheyana, na waisilamu walio wengi hawahusiki kwa lolote katika matukio ya utumiaji nguvu ambayo baadhi yake yanahusika na waisilamu. Kama muislamu yeye mwenyewe binafsi akifanya tendo la kigaidi, mtu huyo atakuwa na hatia ya kuvunja sheria za kiisilamu.

---

[1] Saheeh Muslim, #2422, pia katika: Saheeh Al-Bukhari, #2365.
[2]Saheeh Muslim, #1955, na Al-tirmizi #1409.

# Haki za Binadam na Uadilifu katika Uislamu

Uislamu unatoa haki nyingi za binadamu kwa kila mtu. Zifuatazo ni baadhi ya haki za binadamu zinazolindwa na Uislamu.

Maisha na mali ya kila raia vinazingatiwa kuwa ni vitu vitakatifu katika dola ya Kiisilamu, sawa mtu huyo awe ni Muislamu au la. Vilevile Uislamu unachunga heshima ya mtu. Kwa hivyo katika Uislamu, kuwatukana watu wengine au kuwakebehi hairuhusiwi. Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{Hakika damu zenu, mali zenu, na heshima zenu vitu hivyo ni vitu vinavyolindwa.}**[1]

Ukabila hauruhusiwi katika Uislamu, kwani Qur'an inaelezea usawa wa binadamu katika istilahi zifuatazo:

> **﴾Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari﴿ Qur'an, 49:13**

Uislamu unapinga kufanyiwa wema mtu au taifa kwa misingi ya utajiri wake, nguvu au ukabila. Mwenyezi Mungu amewaumba wanadamu wakiwa sawa na kuwa kitu pekee kinachowafanya watu wawe wabora ni misingi ya kiimani imani na uchaji Mungu wao. Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{Enyi watu! Mungu wenu ni**

---

[1] Kitabu: Saheeh Al-Bukhar, #1739, na katika: Mosnad Ahmad, #2037. katika hadithi hii Mtume anamaanisha kuwa Uislamu una haramisha Mauaji na Umwagaji Damu, pia una haramisha Wizi, Unyang'anyaji Uporaji na Udhalimu.

**mmoja na baba yenu (Adam) ni mmoja. Hakuna ubora kwa Mwarabu kuliko asiyekuwa Mwarabu, na hakuna ubora kwa asiyekuwa Mwarabu kuliko Mwarabu, hakuna ubora kwa Mwekundu (Mtu Mweupe aliechanganyika na wekundu) kuliko Mweusi na hakuna ubora kwa Mweusi kuliko Mwekundu,[1] ispokuwa kwa ucha Mungu.}[2]**

Moja ya kero kubwa inayowakabili watu kwa sasa ni ukabila. Ulimwengu ulioendelea unaweza kumpeleka mtu hadi mwezini lakini hauwezi kumzuia mtu asimchukie na kumpiga vita binadamu mwenzake. Tangu enzi za Mtume Muhammad ﷺ Uislamu umeshatoa mfano uliowazi wa namna ya kumaliza ukabila. Safari ya kila mwaka ya kuhiji Maka inaonyesha udugu wa hakika wa kiisilamu wa makabila na mataifa yote, pale ambapo kiasi cha Waisilamu milioni mbili kutoka sehemu zote duniani wanakwenda Maka kuhiji.



Uislamu ni dini ya uadilifu. Mungu amesema:

> **﴾Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu...﴿ Qur'an, 4:58**

Na amesema:

---

[1] Rangi zilizotajwa katika maneno haya ya mtume ni za mifano tu. Maana yake ni kuwa katika usilamu hakuna alie bora kuliko mwengine kwa sababu ya rangi yake, sawa awe mweupe, mweusi, mwekundu, au rangi yoyote ile.

[2] Mosnad Ahmad, #2278.

**❬...Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanao hukumu kwa haki❭ Qur'an, 49:9**

Tunatakiwa tuwe waadilifu hata kwa wale tunaowachukia, kama Mungu alivyosema:

**❬Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu...❭ Qur'an, 5:8**

Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{Enyi watu, jihadharini na dhulma kwani dhuluma itakuwa ni giza katika Siku ya Kiyama.}**[1]

Na wale wasiopata haki zao (wale wenye madai ya haki) katika maisha haya ya dunuia, basi watapata haki zao Siku ya Kiyama, kama alivyosema Mtume ﷺ: **{Hakika mtazirudisha haki kwa wenyewe Siku ya Kiyama (na maovu yatalipiwa fidia)...}**[2]

---

[1] Mosnad Ahmad, #5798, pia angalia, Saheeh Al-Bukhari, #2447.
[2] Saheeh Muslim, #2582, na katika: Mosnad Ahmad, #7163.

# Mwanamke ana Nafasi gani katika Dini ya Kiislamu?

Uislamu unamtazama mwanamke, sawa awe mwanamwali au mke, kuwa ni mtu mwenye haki zake binafsi, akiwa na haki ya kumiliki na kutumia miliki na pato lake bila kusimamiwa na mtu yeyote (awe baba yake, mumewe, au mtu mwengine yeyote). Ana haki ya kununua na kuuza, kutoa zawadi na sadaka, na anaweza kutumia pesa zake apendavyo. Mahari inayotolewa na bwana harusi na kupewa bibi harusi ni kwa ajili ya matumizi binafsi ya bibi harusi, na mwanamke ana haki ya kuendelea kutumia jina la ukoo wake na hatumii jina la mumewe.



Uislamu unamhamasisha kila mume kumtendea wema mkewe, kama alivyosema Mtume Muhammad ﷺ: **{Wabora wenu ni wale walio bora zaidi katika kuwatendea wema wake zao}**[1]

Wakinamama wana heshima kubwa katika Uislamu. Uislamu unahusia watu kuwatendea wema wakinamama. **Mtu mmoja alimwendea Mtume Muhammad ﷺ na akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! ni nani mwenye haki sana kwangu niwe nae karibu zaidi?" Mtume ﷺ akasema: {Mama yako.} Yule mtu akasema: "kisha nani?" Mtume ﷺ akasema: {Kisha Mama yako.} Yule mtu akauliza tena, "Kisha nani?" Mtume ﷺ**

[1] Ibn Majah, #1978, na katika: Al-Tirmizi, #3895.

**akasema: {Kisha Mama yako.} Yule mtu akauliza tena: "Kisha nani?" Mtume ﷺ akasema: {Kisha baba yako.}**[1]

(Tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/women kwa maelezo zaidi juu ya wanawake katika Uislamu.)

## Familia katika Uislamu

Familia, ambayo ni kiungo kikuu cha maisha bora, kwa hivi sasa kimevunjika. Nidhamu ya familia katika Uislamu inaleta haki kwa mume, mke, watoto, na ndugu kwa usawa maridadi. Uislamu unastawisha kuacha tabia za ubinafsi, unaboresha kufanya ukarimu, na mapenzi kwa mfumo wa nidhamu ya familia yenye kushirikiana vizuri. Amani na ulinzi unaotolewa na kikundi cha familia imara unathaminiwa sana, na jambo hilo linachukuliwa kuwa ni msingi wa ukuaji wa kiroho wa wana familia. Nidhamu ya jamii ya kuridhisha inajengwa kwa kuwepo kwa familia kubwa na kwa kuwathamini watoto.

## Waislamu Wanawatendea vipi Wazee?

Katika ulimwengu wa Kiislamu ni nadra kukuta “makazi ya wazee.” Mkazo wa kuwalea wazazi wanapokuwa katika kipindi hiki kigumu katika maisha yao unazingatiwa ni fahari, baraka na ni nafasi ya kukomaa kiroho. Katika Uislamu, haitoshi tu kuwaombea dua wazazi wetu, lakini inatupasa kuwatendea kwa huruma isiyo na mpaka, huku tukiwa tunakumbuka kuwa wakati tulipokuwa watoto hatujiwezi, wawo walitupendelea kuliko walivyojipendelea nafsi zao. Wakina mama wana heshima za pekee. Wazazi wa Kiisilamu

[1] Saheeh Muslim,#2548 na Saheeh al-Bukhari, #5971.

wanapofikia umri wa utu uzima, wanatendewa kwa upole, pamoja na wema na kupewa kipaumbele.

Katika Uislamu, mtu kuwahudumia wazazi wake ni wajibu wa pili baada ya sala, na ni haki yao kutarajia huduma hizo. Na inazingatiwa kuwa ni ufedhuli kutamka neno la kuudhi wakati, inapowawia vigumu kuwavumilia kwa kuwa si makosa yao, ila uzee umekuwa ni jambo zito.

Mwenyezi Mungu amesema:

> **﴾Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa hishima. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni.﴿ Qur'an, 17:23-24.**

## Ni Zipi Nguzo Tano za Uislamu?

Nguzo tano za Uislamu ni mfumo wa maisha ya Muislamu. Nazo ni Ushuhuda wa imani, Sala, kutoa Zaka, (msaada kwa wenye shida), kufunga mwezi wa Ramadhani, na kwenda kuhiji Makka mara moja kwa maisha yote kwa mwenye uwezo.

### 1) Ushuhuda wa imani:

Ushuhuda wa imani ni kusema kwa kusadikisha, "*La ilaha illa Allah, Muhammadur rasulu Allah*" Maneno haya yana maana ya kuwa: "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa Haki ila Mwenyezi

Mungu (Allah)[1], na Muhammad ni Mtume wa Mungu." Sehemu ya kwanza, "Hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu," inamaanisha kuwa, hakuna kiumbe yeyote mwenye haki ya kuabudiwa ispokuwa Mwenyezi Mungu peke yake, na kuwa Mungu hana mshirika wala mwana. Huu ushuhuda wa imani unaitwa ***Shahada***, ambayo ni njia nyepesi inatakiwa kutamkwa kwa kusadikisha ili ubadilike na kuingia Uislamu Ushuhuda wa imani ni nguzo ya Kiislamu iliyo muhimu sana.

## 2) Sala:

Waislamu wanasali Sala tano kwa siku. Kila Sala haichukui zaidi ya dakika chache kuitekeleza. Sala katika Uislamu ni kiunganishi cha moja kwa moja kati ya mwenye kusali na Mungu. Hakuna muunganishi kati ya Mungu na mwenye kuabudu.

Katika sala, mtu anahisi furaha ya moyoni, amani, na raha, na kuwa Mwenyezi Mungu amemridhia. Mtume Muhammad ﷺ amesema: **{Ewe Bilali waite watu waje kusali, wacha tuburudike na sala.[2]}** Bilali alikuwa ni mmoja wa maswahaba wa Muhammad ﷺ ambaye alipewa jukumu la kuwaita watu kwenda kusali.

Sala husaliwa alfajiri, adhuhuri, alasiri, magharibi na ishaa. Muislamu anaweza kusali, takribani, popote pale, kwa mfano mashambani, maofisini, viwandani, au vyuoni.

(Tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/prayer kwa maelezo zaidi kuhusu sala katika Uislamu.)[3]

---

[1] Kwa maelezo zaidi kuhusiana na neno Allah tazama kifungu cha mwisho katika ukurasa wa 65

[2] Kitabu: Abu-Dawood, #4985, na katika Mosnad Ahmad, #2278.

[3] Au rejea kitabu kiitwacho A guide to Prayer in Islam by M.A.K saqib. Kwa kujipatia nakala tafadhali tembelea mtandao uliotajwa hapo juu.

## 3) Kutoa Zaka (Msaada kwa Masikini, wenye shida):


Kila kitu kinamilikiwa na Mungu, kwa hivyo utajiri unaomilikiwa na watu ni amana juu yao. Maana asilia za neno ***Zakat*** ni mbili 'utakaso' na 'kukua' kutoa zaka, maana yake ni 'kutoa asilimia maalum kutoka katika vitu maalumu kuyapa makundi maalumu ya watu wenye shida.' Asilimia zinazolazimika kutolewa kwa umiliki wa dhahabu, madini ya fedha, au pesa taslimu ambazo zimefikia kiasi cha gramu 85 za dhahabu na zimekuwa katika milki yake kwa mwaka mmoja wa miezi miandamo ni asilimia mbili na nusu ya mali hizo. Milki zetu zinatakaswa kwa kuzitengea fungu dogo la kuwapa wenyeshida, na tendo hilo ni sawa sawa na kuondosha matawi yaliochakaa ili kuacha mti ustawi vizuri, kwani kufanya hivyo ni kuupa balanzi mmea na kuupa nguvu mpya ya kukua.



Vile vile, mtu anaweza kutoa zaidi kwa kadri anavyopenda hiyo ikiwa ni sadaka ya hiari au mchango wa kusaidia mambo ya kheri.

## 4) Kufunga mwezi wa Ramadhani:

Kila mwaka katika mwezi wa Ramadhani,[1] Waislamu wanafunga kuanzia alfajiri mpaka kuzama kwa jua, wakijizuia na kula, kunywa, na mahusiano ya kingono.




[1] Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni Mwezi wa tisa wa Kalenda ya kiislamu (ambawo ni mwezi wa muandamo)

Ingawa funga ina faida kwa afya, pia kimsingi inazingatiwa kuwa ni utaratibu muhimu wa kujitakasa kiroho. Kwa kujizuia na raha za dunia, hata kwa muda mfupi, mfungaji anajipatia huruma ya kweli ya kuwaonea wale wenye njaa, vile vile anapevuka katika maisha yake ya kiroho.

## 5) Kwenda kuhiji Makka:

Hija ya kila mwaka kuelekea Maka ni lazima mara moja kwa umri wote kwa wale wenye uwezo wa kimwili na kiuchumi wa kutekeleza jambo hilo. Kiasi cha watu milioni mbili huenda Makka

*Mahujaji wakiwa wanaswali ndani ya Msikiti wa Haram (Msikiti Mtukufu wa Maka) katika Msikiti huu kunapatikana Kaaba ( jengo jeusi katika picha) ambayo Waislamu huelekea wanapokuwa wanaswali. Kaaba ni sehemu ya Ibada ambayo Mwenyezi Mungu alimuamrisha Nabii Ibrahim na mwanawe, Nabii Ismail, kuijenga.*



kila mwaka wakitokea kila pembe ya dunia. Ingawa siku zote Makka inajazwa na wageni, Hija ya kila mwaka hufanyika katika mwezi wa kumi na mbili wa kalenda ya Kiislamu. Mahujaji wa kiume huvaa nguo maalumu za hali ya chini zinazoondosha tofauti za kitabaka na kitamaduni kiasi ambacho watu wote wanasimama wakiwa ni sawa sawa mbele ya Mungu.

Ibada za hija zinakusanya kuzunguka Kaaba mara saba na kutembea baina ya milima ya Safa na Marwa mara saba, kama alivyofanya Bibi Hajar alipokuwa anatafuta maji. Kisha mahujaji wanasimama pamoja katika Arafa[1] na wanamuomba Mungu awape

[1] eneo lililo umbali wa maili 15 kotoka Maka.

kile wanachokitaka na wanamuomba msamaha, katika hali ambayo mara nyingi inadhaniwa kuwa ni onyesho la kwanza la Siku ya Kiyama.

Mwisho wa hija unakamilishwa kwa Sikukuu ya Mfunguo Tatu, ambayo husheherehekewa kwa sala. Idi hii na Idi ya Mfunguo Mosi, sikukuu ya ukumbusho wa kuisha kwa Ramadhani, hizi ndizo sikukuu mbili za kila mwaka za kalenda ya Kiislamu.

(Tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/pillars kwa maelezo zaidi kuhusu nguzo tano za Kiisilamu.)

## Uislamu Nchini Marekani

Ni vigumu kutoa kauli ya jumla kuhusu Waislamu wa Marekani. Wao ni watu waliosilimu, wahamiaji, wafanyakazi za viwandani, na madakitari. Jamii hii iliyo na hali mbalimbali inaunganishwa na imani moja, wakiimarishwa na mtandao wa taifa zima wa idadi kubwa ya misikiti. Waislamu walifika Amerika ya Kaskazini mapema. Katika kipindi cha karne ya kumi na nane, kulikuwa na Waisilamu wengi katika eneo la Amerika ya Kaskazini.



Idadi kubwa ya Wamarekani wameingia katika zizi la dini ya Kiislamu. Watu hao ni wa kutoka tabaka mbalimbali: matajiri, masikini, wasomi, na watu wasio kuwa wasomi. Hivi leo kuna kiasi cha Waislamu milioni tano na nusu nchini Marekani.[1]

❊❊❊

[1] *The World Almanac and book of facts* cha mwaka mwaka 1996, Famigheti, ukurasa wa, 644.

# Kwa Maelezo  Zaidi Kuhusu Uislamu



Kama utapenda kujua maelezo zaidi kuhusu Uislamu, au kama una swali lolote au mawazo yeyote, au kitabu hiki kwa lugha nyenginezo, tafadhali tembelea mtandao wa kitabu hiki:

www.islam-guide.com

Kwa kujipatia nakala ya kitabu hiki, tafadhali tembelea: www.islam-guide.com/copies

Pia, unaweza kuwasiliana na moja ya taasisi zifuatazo:

**1) Marekani:**

**Islamic Assembly of North America**
3588 Plymouth Road, Suite # 270,
Ann Arbor, MI 48105, USA
Tel.: (734) 528-0006 - Fax: (734) 528-0066
E-mail: IANA@IANAnet.org

**Islamic Foundation of America**
PO Box: 3415, Merrifield, VA 22116, USA
Tel.: (703) 914-4982 - Fax: (703) 914-4984
E-mail: info@ifa.ws

**Alharamain Islamic Foundation**
1257 Siskiyou Blvd., no. 212,
Ashland, OR 97520, USA
Tel.: (541) 482-1116 - Fax: (541) 482-1117
E-mail: haramain@alharamain.org

**Islamic information institute of Dar-us-Salam**
5301 Edgewood Rd., College Park, MD 20740-4623, USA
Tel.: (301) 982-9463 – Fax: (703) 982-9849
E-mail: iii@islamworld.net

**World Assembly of Muslim Youth**
PO Box: 8096, Falls Church,
VA 22041-8096, USA
Tel.: (703) 820-6656 - Fax: (703) 783-8409
E-mail: support@wamyusa.org

Al Jumuah Magazine
PO Box: 5387, Madison,
WI 53705-5387, USA
Tel.: (608) 277-1855 - Fax: (608) 277-0323
E-mail: info@aljumuah.com

Note: Tafadhali tembelea **www.islam-guide.com/centers** kwa kujipatia anuani za vituo vya kiisilamu vilvyo karibu yako.

## 2) Canada:

**Islamic Information & Da'wah Center International**
1168 Bloor Street West, Toronto,
Ontario M6H 1N1, Canada
Tel.: (416) 536-8433 - Fax: (416) 536-0417
E-mail: comments@islaminfo.com

## 3) Uingereza (UK):

**Al-Muntada Al-Islami Centre**
7 Bridges Place, Parsons Green, London SW6 4HW, UK
Tel.: 44 (0207) 736 9060 Fax: 44 (0207) 736 4255
E-mail: muntada@almuntada-alislami.org

Jam'iat Ihyaa' Minhajaj Al-Sunnah
PO Box: 24, Ipswich, Suffolk IP3 8ED, UK
Tel. and Fax: 44 (01473) 251578
E-mail: **mail@jimas.org**

## 4) Saudi Arabia:

**Alharamain Islamic Foundation**
PO Box: 69606, Riyadh 11557, Saudi Arabia
Tel.: (966-1) 465-2210 - Fax: (966-1) 462-3306
E-mail: haramain@alharamain.org

**World Assembly of Muslim Youth**
PO Box: 10845, Riyadh 11443, Saudi Arabia
Tel.: (966-1) 464-1669 - Fax: (966-1) 464-1710
E-mail: info@wamy.org

## Egypt:

**IslamicConveying Islamic Message Society**
PO Box: 834, Alex – Egypt
E-mail: **info_en@islamic-message.net**
E-mail: **cims_eg@yahoo.com**
Site: www.islamic-message.net

# Kwa ushauri na maoni juu ya kitabu Hiki

Ikiwa una mapendekezo yoyote au maoni juu ya kitabu hiki, tafadhali yatume kwa mtunzi, I. A. Ibrahim kupitia
E-mail: ib@i-g.org Tel.: (966-1) 454-1065 . Fax: (966-1) 453-6842
P.O.Box 21679, Riyadh 11485, Saudi Arabia.

Pia, ukitaka maelezo zaidi kuhusu Uislamu au kama ukitaka nakala za ziada za kitabu hiki unaweza kuwasiliana na mtunzi.

## Kwa kijisomea zaidi kuhusu Uislamu

*The True Religion*, by Bilal Philips.
*This is the truth*, published by Alharamain Islamic Foundation.
*The Qurani and the Modern Science*, by Dr. Maurice Bucaille, edited by Dr. A.A.B Philips.
*Towards Understanding Islam*, by Abul A'la al-Mawdudi.(Ipo tafsiri yake inayoitwa *(Misingi ya Uislamu)* inauzwa madukani nchini Tanzania
*Life after death* (pamphlet), by World Assembly of Muslim Youth.
*The Muslim's Belief*, by Muhammad Al-Uthaimin, translated by Dr. Maneh al-Johani.
*Interpritation of the Meaning of The Noble Qur'an in the English Language*, by Dr. Muhammad al-Hilali and Dr. Muhammad Khan.
Kwa kujipatia nakala ya kitabu chochote katika hivyo au kujipatia vijitabu, tafadhali tembelea www.islam-guide.com/books au wasiliana na moja ya taasisi zilizoorodheshwa katika ukurasa wa 70-71-72)

## Vitabu vya Marejeo

Ahrens, C. Donald. 1988. Meteorology Today. 3rd ed. St. Paul: West Publishing Company.

Anderson, Ralph K.; and others. 1978. The Use of Satellite Pictures in Weather Analysis and Forecasting. Geneva: Secretarial of the World Meteorological Organization.

Anthes, Richard A.; John J. Cahir; Alistair B. Fraser; and Hans A. Panofsky. 1981. The Atmosphere. 3rd ed. Columbus: Charles E. Merrill Publishing Company.

Barker, Kenneth; and others. 1985. The NIV Study Bible, New International Version. Grand Rapids, Michigan: Zondervan

Publishing House.

Bodin, Svante. 1978. Weather and Climate. Poole, Dorest: Blandford Press Ltd.

Cailleux, Andre’. 1968. Anatomy of the Earth. London: World University Library.

Couper, Heather; and Nigel Henbest. 1995. The Space Atlas. London: Dorling Kindersley Limited.

Davis, Richard A., Jr. 1972. Principles of Oceanography. Don Mills, Ontario: Addison-Wesley Publishing Company.

Douglas, J. D.; and Merrill C. Tenney. 1989. NIV Compact Dictionary of the Bible. Grand Rapids, Michigan: Zondervan Publishing House.

Elder, Danny; and John Pernetta. 1991. Oceans. London: Mitchell Beazley Publishers.

Famighetti, Robert. 1996. The World Almanac and Book of Facts 1996. Mahwah, New Jersey: World Almanac Books.

Gross, M. Grant. 1993. Oceanography, a View of Earth. 6th ed. Englewood Cliffs: Prentice-Hall, Inc.

Hickman, Cleveland P.; and others. 1979. Integrated Principles of Zoology. 6th ed. St. Louis: The C. V. Mosby Company.

Al-Hilali, Muhammad T.; and Muhammad M. Khan. 1994. Interpretation of the Meanings of The Noble Quran in the English Language. 4th revised ed. Riyadh: Maktaba Dar-us-Salam.

The Holy Bible, Containing the Old and New Testaments (Revised

Standard Version). 1971. New York: William Collins Sons & Co., Ltd.

Ibn Hesham, Abdul-Malek. Al-Serah Al-Nabaweyyah. Beirut: Dar El-Marefah.

The Islamic Affairs Department, The Embassy of Saudi Arabia, Washington, DC. 1989. Understanding Islam and the Muslims. Washington, DC: The Islamic Affairs Department, The Embassy of Saudi Arabia.
Kuenen, H. 1960. Marine Geology. New York: John Wiley & Sons, Inc.

Leeson, C. R.; and T. S. Leeson. 1981. Histology. 4th ed. Philadelphia: W. B. Saunders Company.

Ludlam, F. H. 1980. Clouds and Storms. London: The Pennsylvania State University Press.

Makky, Ahmad A.; and others. 1993. Ee'jaz al-Quran al-Kareem fee Wasf Anwa' al-Riyah, al-Sohob, al-Matar. Makkah: Commission on Scientific Signs of the Quran and Sunnah.

Miller, Albert; and Jack C. Thompson. 1975. Elements of Meteorology. 2nd ed. Columbus: Charles E. Merrill Publishing Company.

Moore, Keith L.; E. Marshall Johnson; T. V. N. Persaud; Gerald C. Goeringer; Abdul-Majeed A. Zindani; and Mustafa A. Ahmed. 1992. Human Development as Described in the Quran and Sunnah. Makkah: Commission on Scientific Signs of the Quran and Sunnah.

Moore, Keith L.; A. A. Zindani; and others. 1987. Al-E'jaz al-Elmy fee al-Naseyah (The scientific Miracles in the Front of the Head). Makkah: Commission on Scientific Signs of the Quran and Sunnah.

Moore, Keith L. 1983. The Developing Human, Clinically Oriented Embryology, With Islamic Additions. 3rd ed. Jeddah: Dar Al-Qiblah.

Moore, Keith L.; and T. V. N. Persaud. 1993. The Developing Human, Clinically Oriented Embryology. 5th ed. Philadelphia: W. B. Saunders Company.

El-Naggar, Z. R. 1991. The Geological Concept of Mountains in the Quran. 1st ed. Herndon: International Institute of Islamic Thought.

Neufeldt, V. 1994. Webster's New World Dictionary. Third College Edition. New York: Prentice Hall.

The New Encyclopaedia Britannica. 1981. 15th ed. Chicago: Encyclopaedia Britannica, Inc.

Noback, Charles R.; N. L. Strominger; and R. J. Demarest. 1991. The Human Nervous System, Introduction and Review. 4th ed. Philadelphia: Lea & Febiger.

Ostrogorsky, George. 1969. History of the Byzantine State. Translated from the German by Joan Hussey. Revised ed. New Brunswick: Rutgers University Press.

Press, Frank; and Raymond Siever. 1982. Earth. 3rd ed. San Francisco: W. H. Freeman and Company.

Ross, W. D.; and others. 1963. The Works of Aristotle Translated into English: Meteorologica. vol. 3. London: Oxford University Press.

Scorer, Richard; and Harry Wexler. 1963. A Colour Guide to Clouds. Robert Maxwell.

Seeds, Michael A. 1981. Horizons, Exploring the Universe. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Seeley, Rod R.; Trent D. Stephens; and Philip Tate. 1996. Essentials of Anatomy & Physiology. 2nd ed. St. Louis: Mosby-Year Book, Inc.
Sykes, Percy. 1963. History of Persia. 3rd ed. London: Macmillan & CO Ltd.

Tarbuck, Edward J.; and Frederick K. Lutgens. 1982. Earth Science. 3rd ed. Columbus: Charles E. Merrill Publishing Company.

Thurman, Harold V. 1988. Introductory Oceanography. 5th ed. Columbus: Merrill Publishing Company.

Weinberg, Steven. 1984. The First Three Minutes, a Modern View of the Origin of the Universe. 5th printing. New York: Bantam Books.

Al-Zarkashy, Badr Al-Deen. 1990. Al-Borhan fee Oloom Al-Quran. 1st ed. Beirut: Dar El-Marefah.

Zindani, A. A. This is the Truth (video tape). Makkah: Commission on Scientific Signs of the Quran and Sunnah.

Tuki, English-Swahili Dictionary Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili, ya Institute of Kiswahili Research University of Dar es Salaam 1996.

Kamusi ya Al-Muujamul al-Wajiizi ya Baraza la Lugha ya Kiarabu iliyochapishwa na wizara ya malezi na elimu mwaka 1417 h. Sawa na 1996 a.d, a. R. Egypt.

Cambridge, International Dictionary of English.1997 ad.

# Nambari za hadithi[1]

Nambari za hadithi zilizo katika kitabu hiki zinategemea mambo yafuatayo:

- Saheeh Muslim: kwa kulingana na namba za Muhammad F. Abdul-Baqy.
- Saheeh Al-Bukhari: kwa kulingana na namba za Fath Al-Bari.
- Al-Tirmizi: kwa kulingana na namba za Ahmad Shaker.
- Mosnad Ahmad: kwa kulingana na namba za Dar Ehya'Al Torath Al-Araby, Beirut.
- Mowatta' Malek: kwa kulingana na namba za Mowatta' Malek.
- Abu-Dawood: kwa kulingana na namba za Muhammad Muhyi Al-Deen Abdul-Hameed.
- Ibn Majah: kwa kulingana na namba za Muhammad F. Abdul-Baqy.
- Al-Daremey: kwa kulingana na namba za Khalid Al-Saba Al-Alamy na Fawwaz Ahmad Zamarly.

✵ ✵ ✵

[1] **Hadithi, ambazo ni habari zilizonukuliwa kwa njia za kuaminika na wafuasi wa Mtume Muhammad ﷺ habari za kile alichosema, tenda au kukiafiki.**